# Nipashe

Alhamisi Januari 14, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580460

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




ama

ALHAMISI JANUARI 14, 2021

AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 12

Kinachofanikisha wenyeji wa Kagera wasisukumwe kusaka chanjo watoto

Ukurasa 13

MGANGA MKUU WA SERIKALI:

Sasa kazi, tuone vitendo kila mmoja akiwajibikia wagonjwa

LATRA: Tunatamani tusahau ajali kupitia vidhibiti mwendo kila basi

•Kasi, mbwembwe njiani, uegeshaji ovyo

Na Sabato Kasika

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), linasema watu 3,400 wanapoteza maisha kila siku duniani kupitia ajali za barabarani, huku dira ya ripoti yake ya usalama barabarani kuanzia 2011 hadi mwaka jana, iliangaza kufuta nusu ya ajali, majeruhi na vifo.

Ni tatizo linalogusa maisha ya watu hata kitaifa, mfano hai ikirejewa kauli za mwanzo za Inspekta Jenerali wa Polisi Mstaafu, Said Mwema, aliwahi kueleza hatua ya mafanikio kudhibiti uhalifu katika siku zake za mwanzo, lakini akikiri kutiwa ukakasi wa kusumbuliwa na usalama barabarani.

Kimsingi, usalama wa barabarani ni suala mtambuka lisiloishia mkononi mwa polisi pekee, bali linagusa mamlaka zingine za kiserikali na zisizo za kiserikali zinazosimamia usalama huo, kuanzia sheria hadi utendaji, abiria, madereva na watumia barabara.

WHO inaitaja ajali kuwa jambo linalowaacha pia waathirika katika ulemavu wa kudumu kimaisha na kuathiri mustakabali wa familia nyingi duniani, huku vifo hivyo vya ghafla vikiacha makovu ya kudumu kwa familia.

Inazitaja athari hizo ni kuwaacha majeruhi kila kona ya dunia na inaongeza mamilioni wanaosalia kuwa tegemezi wa kudumu katika baadhi ya mambo, kutokana na athari hizo.

Picha kuhusu yanayojiri barabarani na kelele za vidhibiti mwendo. PICHA: MTANDAO.

Kinachofanywa na WHO ni sehemu ya kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's), mahususi Namba Tatu, linalohusu afya na ustawi wa watu kwa rika zote ifikapo 2030.

Ni lengo linalohusu ambalo katika mustakabali wake mpana, unaangukia kupunguza vifo vya mama wajawazito, pia watoto wanaozaliwa.

Kuna hatua mbalimbali ambazo serikali na wadau zimeshachukua katika tafsiri na lengo la ama kupunguza au kumalizika kabisa nchini.

Hapo inajumuisha ushuhuda kama vile kuweka mfumo wa kisatelaiti wa kufuatilia mwenendo wa magari barabarani uitwao 'Vehicle Tracking System' (VTS), ambao unaofanana na mifumo iliyopo kwenye magari.

VIDHIBITI MWENDO

Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri wa Barabara (LATRA), Johansen Kahatano, anasema hadi kufika mwishoni mwa mwaka jana, takribani mabasi 5,000 ya safari ndefu kivuka mikoa na mipaka ya nchi, yalifungiwa mfumo huo.

Kahatano anasema, licha ya kuendelea kuwapo matukio ya ajali barabarani, kwa kiasi kikubwa mfumo huo umepunguza ajali zilizosababisha vifo na majeruhi wengi nchini.

"Kufungwa mfumo huo kwenye baadhi ya mabasi, malalamiko ya abiria kuhusu madereva kuendesha vibaya yamepungua na hayajitokezi sana kama zamani," anasema Kahatano.

Pia, anafafanua kuwa ni mfumo unaorahisishia ufuatiliaji, kupata taarifa sahihi na za haraka, zitokanazo na mwenendo wa madereva kila kona ya nchi.

"Wito wangu ni kwa baadhi ya wamiliki wa mabasi wote wabadilike ili tusaidiane katika vita hii ya kudhibiti ajali, wahakikishe madereva hawachezei mfumo huo katika mabasi yao," anaeleza.

Anafafanua mfumo huo unavyofanya kazi, kwamba inarekodi spidi kuanzia dereva atakavyoendesha, lakini mwendokasi unapofika kasi ya kilomita 85 kwa saa, kengele hulia kumtahadharisha mwendeshaji.

"Mfumo huu unaruhusu ufuatiliaji wa basi wakati huo huo likiwa safarini, kwani ofisa wa LATRA, mmiliki au Jeshi la Polisi, wanaweza kukaa ofisini na kufuatilia kila basi mwenendo wake na kuchukua hatua kwa wakati," anasema.

Kahatano, anafafanua kuwa, mfumo haulizuii gari kuvuka spidi iliyowekwa, lakini unahifadhi rekodi za kasi barabarani, mahali na muda anaosimama njiani.

WANAOTETEA ABIRIA

Hassan Mchanjama, Mwenyekiti wa Chama cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA), anaeleza kuunga mkono juhudi zinazofanywa na wadau wa usafiri kusaka usalama wa abiria.

"Kama wadau wa usafiri, tunaunga mkono juhudi za kuhakikisha abiria anasafiri na kufika salama kule aendako na pia apate huduma sahihi, hivyo suala la VTS na tiketi za kielektroniki ni vya muhimu," anasema Mchanjama.

Anafafanua: "Tunaamini kwamba kuna mafanikio kwenye mfumo huo, ingawa zipo changamoto mbalimbali hasa zinazotokana na baadhi ya wamiliki wa mabasi kutotumia au kutofuatilia madereva wao, ili wasichezee mfumo huo katika mabasi yao."

Kuhusu ukatishaji tiketi za mabasi kwa njia za kielektroniki, anakiri kukubaliana na mfumo huo mpya, jambo wanaoamini itawaondolea abiria usumbufu wa walio nao kila mara.

"Hatua hii ya kuwapo tiketi hizo itaondoa wapigadebe vituoni, pia itakomesha wajanja wachache ambao wamekuwa wakipandishia abiria nauli kwa kujali maslahi yao zaidi," anasema.

Mwenyekiti huyo anasema, chama chao kimekuwa kikitoa elimu kwa abiria kujua haki zao, kuanzia usalama katika safari na hata kuepuka kuibiwa mali au kuzindishiwa nauli wanapotaka kukata tiketi.

UKURASA 11

## WALIONASWA utumikishaji wenye ulemavu kushtakiwa utakatishaji

UKURASA 2



## DOLA milioni 425 kuboresha elimu ya juu Tanzania

UKURASA 3

# Gari la maiti lakamatwa na dawa kulevya katika jeneza

UKURASA 2



# Watumishi wa MOI matatani kuchepusha dawa za bilioni 1.2/-

UKURASA 2

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Brigedia Jenerali John Mbungo akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa taarifa ya taasisi yake kufanikiwa kudhibiti uchepushaji na ubadhirifu wa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.2. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wahamiaji haramu wakutwa hoi

UKURASA 3

**MICHEZO** **IBENGE AJITOA SIMBA, AITANGAZIA VITA CAF** UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

HABARI KITAIFA

## Watumishi MOI matatani madai uchepushaji dawa

**Na Beatrice Shayo**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imewatia matatani wafanyakazi 23 wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) kwa tuhuma za kuchepusha dawa zenye gharama ya Sh. bilioni 1.2.

Wafanyakazi wanaodaiwa kufanya hujuma hiyo ni wa idara ya famasia katika taasisi hiyo na wanahojiwa na TAKUKURU huku wakitakiwa kurejesha fedha hizo.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam kuwa wameokoa hujuma hiyo kwa kushirikiana na uongozi wa MOI.

Alisema uchepushwaji huo ulifanywa kupitia mfumo wa kutunza taarifa za kumbukumbu za utoaji wa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa (MEDPRO4) unaotumika katika taasisi hiyo.

Mbungo alisema ubadhirifu huo umedhibitiwa baada ya uchunguzi kubaini tofauti kati ya taarifa za dawa zilizoingizwa na wafamasia kwenye mfumo huo na taarifa zilizoandikwa na madaktari kwenye majalada ya wagonjwa.

"Daktari akiandika dawa 30 kwa ajili ya matumizi ya mgonjwa kwa muda wa mwezi, mfamasia anaongeza idadi ya dawa na kuingiza kwenye mfumo wa dawa 60 ambazo ni tofauti na zilizotolewa, jambo ambalo katika uhalisia mgonjwa hajapatiwa idadi hiyo ya dawa," alisema.

Pia alisema wamebaini kuwapo kwa watumishi wa kitengo hicho wanaofanya ubadhirifu wa kuongeza dawa zenye bei kubwa kwenye fomu za madaktari tofauti na maelekezo yanayotolewa.

Mbungo alisema uchunguzi huo umebaini wafamasia hao walisababisha upotevu wa dawa kwa kuingiza taarifa za uongo kwenye mfumo zinazoonyesha mgonjwa amepatiwa dawa ya aina moja zaidi ya mara moja.

Alisema Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alikuwa akifuatilia utendaji wa maduka ya dawa katika kila hospitali tangu alipoingia madarakani na kubaini tatizo hilo.

Katika maduka ya dawa, alisema hakuna kumbukumbu sahihi za uombaji wa dawa na utoaji na kwamba jambo hilo alilibaini katika hospitali za Busekelo mkoani Mbeya, Dodoma na Katavi.

Mbungo alisema TAKUKURU itaendelelea kuwa macho kufuatilia wale wote wanaojihusisha na ubadhirifu wa aina hiyo na amewataka wale wanaohusika na huduma za utoaji wa dawa kuwa mfano wa MOI ili kwa pamoja kudhibiti uchepushaji wa aina hiyo.

# Gari la maiti lakamatwa na dawa kulevya katika jeneza

**Na Boniface Gideon,** TANGA

KIKOSI Maalum cha Jeshi la Polisi mkoani Tanga, kimenasa dawa za kulevya zenye uzito wa kilogramu 133 (mabunda 1,685) zikisafirishwa huku zikiwa zimefichwa ndani ya mifuko sita ya sandarusi iliyowekwa kwenye gari la kusafirishia maiti.

Limesema mifuko hiyo ya sandarusi yenye dawa hizo imekutwa ndani ya jokofu ambalo huwekwa jeneza lenye mwili wa marehemu.

Akizungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi mkoani Tanga, Kamishna Msaidizi Blasius Chatanda, alisema jana kuwa dawa hizo zilikamatwa Januari 12 mwaka huu majira ya saa mbili usiku katika Kijiji cha Manga, Kata ya Mkata, Wilaya ya Handeni.

Alisema gari lililohusika kusafirisha dawa hizo ni aina ya Volvo lenye namba za usajili T 569 DSZ, mali ya Kampuni ya Nuru Funeral Service ya Dar es Salaam.

"Tuliyemkamata ni dereva wa gari hilo la kubeba maiti, Simon Tarimo (37), mkazi wa Kimara, Dar es Salaam. Huyu alikuwa akisafirisha mirungi akiwa ameweka kwenye jokofu linalotumika kuhifadhia jeneza lenye maiti wakati wa kusafirisha.

"Hizo dawa za kulevya, zilikuwa zimehifadhiwa kwenye mifuko sita ya sandarusi," kamanda huyo alisimulia.

Kwa mujibu wa Kamanda Chatanda, dawa hizo zilikuwa zikisafirishwa kutoka Usangi, Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro kwenda jijini Dar es Salaam.

"Mbinu iliyotumika ni kuweka mifuko kwenye jokofu linalowekwa jeneza, ni kinyume cha matumizi ya gari hilo," kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi alionya.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) nchini Tanzania, Tirso Dos Santos (wa pili kushoto), Ikulu jijini Zanzibar jana. Kushoto ni Ofisa wa Utamaduni UNESCO Tanzania, Nancy Lazaro Mwaisaka. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Walionaswa utumikishaji wenye ulemavu kushtakiwa utakatishaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SAKATA la utumikishwaji watu wenye ulemavu kama ombaomba limechukua sura mpya baada ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuridhia watuhumiwa 13 kushtakiwa kwa mashtaka matano ikiwamo utakatishaji fedha haramu.

Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, kupitia taarifa yake aliyoitoa jana kwa vyombo vya habari, alisema mwezi huu amepokea majalada mbalimbali kutoka vyombo vya upelelezi kwa ajili ya kuyapitia na kufanya uamuzi wa kufungua au kutofungua mashtaka likiwamo sakata hilo.

Alitaja mashtaka mengine yatakayowakabili watuhumiwa hao kuwa ni kujihusisha na uhalifu wa kupangwa kinyume cha Sheria ya Kuzuia Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa Sura ya 200 marejeo ya mwaka 2019.

"Mashtaka mengine ni usafirishaji haramu wa binadamu kinyume cha Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu Na. 6 sita ya mwaka 2008, kushindwa kulipa kodi, ambapo katika nyumba ya kulala wageni ya Madiba ilibainika haikuwa na leseni na hivyo kukwepa kodi kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Kodi sura ya 438 marejeo ya mwaka 2019," alisema.

Mganga alisema shtaka la tano ni kuisababishia Mamlaka ya Serikali hasara kinyume na Sheria ya Kuzuia Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa sura ya 200 marejeo ya mwaka 2019.

Alifafanua kuwa ameridhia mashtaka hayo kutokana na ushahidi uliokusanywa kutoka Jeshi la Polisi ambalo lilipokea taarifa kuwapo kwa nyumba za kulala wageni zinazohifadhi watu wenye ulemavu kutoka mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Geita, Morogoro, Kagera na Tabora waliosafirishwa kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya shughuli ya kuombaomba.

Mkurugenzi huyo alisema baada ya kupitia jalada husika alibaini watu hao wenye ulemavu, watoto wadogo na baadhi wakiwa na ulemavu wa akili walikuwa wamehifadhiwa katika nyumba za kulala wageni ambazo ni mali ya Sadikiel Metta na zilikutwa zikiwa na watu wenye ulemavu 23.

Alisema watuhumiwa hao walikuwa wakiwasukuma watu hao kwa kutumia baiskeli maalum ili kujipatia fedha ya biashara hiyo haramu.

Mkurugenzi huyo alisema nyumba hizo za kulala wageni ni bubu na walikuwa wakipokewa na kupewa hifadhi na Sadikiel Metta ili kujipatia kipato kupitia biashara hiyo haramu.

"Baada ya kuzingatia ushahidi uliokusanywa pamoja na masharti ya Katiba na Sheria mbalimbali zinazoniongoza nimeridhia mashtaka yafuatayo dhidi ya watuhumiwa 13," alisema.

Katika hatua nyingine, DPP ameridhia mashtaka matano dhidi ya askari polisi mkoani Arusha William Alfred na mkewe Dorcus Memruth kwa tuhuma za kujiunganishia umeme kinyume na sheria na kukutwa na dawa za kulevya mkoani humo.

Alitaja mashtaka aliyoridhia kuwa ni kuingilia mfumo wa utoaji huduma muhimu kinyume na Sheria ya Kuzuia Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa kupangwa sura ya 200 marejeo ya mwaka 2019.

"Kupatikana na mimea iliyopigwa marufuku kinyume na Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Dawa za Kulevya Sura ya 95 marejeo ya mwaka 2019, kupatikana na pombe haramu kinyume na sheria ya uthibiti wa pombe za kienyeji, kutumia udanganyifu wa alama za bidhaa kinyume na sheria ya alama za biashara," alisema.

Pia alisema shtaka jingine ni kupatikana na vifungashio vya plastiki vilivyopigwa marufuku.

## HABARI KITAIFA

# Wahamiaji haramu wakamatwa wakiwa hoi



Kundi la Waethiopia 61 walionaswa na Jeshi la Polisi, wakisafirishwa kwa lori kuelekea nchini Malawi wakiwa chini ya ulinzi katika Kituo Kikuu cha Polisi jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limewanasa wahamiaji haramu 61 raia wa Ethiopia wakiwa wanasafirishwa kwenda nchi jirani ya Malawi kwa kutumia lori la mizigo, huku dereva wa gari hilo pia akishikiliwa kwa kosa la kusafirisha wahamiaji hao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, katika Kituo Kikuu cha Polisi cha Mkoa wa Mbeya, Kaimu Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Jerome Ngowi, alisema wahamiaji hao walikamatwa juzi katika kizuizi cha magari, Kijiji cha Gari Jembe barabara kuu ya Tanzania na Malawi. Alisema wahamiaji hao walikuwa wamefichwa kwenye lori aina ya Scania yenye namba za usajili T. 509 AZZ ambalo lilikuwa linaendeshwa na Rabdi Ramadhani (48), mkazi wa Unga Limited, mkoani Arusha.

Alisema maaskari waliokuwapo kwenye kizuizi hicho, walimsimamisha dereva huyo ili wakague gari hilo na walipomhoji kuhusu mizigo aliyobeba alisema amebeba bidhaa za dukani.

Kamanda Ngowi alisema maaskari hao walimlazimisha dereva kufungua mlango wa nyuma wa gari hilo na kubaini alikuwa amewabeba wahamiaji hao.

Alisema mbinu aliyotumia dereva huyo ni kupanga maboksi kadhaa ya bidhaa za dukani mlangoni pamoja na mapipa na kuwaficha wahamiaji hao ndani ili wasionekane.

"Dereva huyu baada ya kubaini kuwa amegundulika, alianza kuwashawishi maaskari wapokee rushwa ya Sh. 3,000,000, lakini kwa sababu ya maadili yao walikataa, alipanda mpaka Sh. milioni 30 bado walikataa na wakamkamata," alisema Kamanda Ngowi.

Alisema baada ya kumhoji dereva wa gari hilo alisema alikuwa anawapeleka katika mji wa Kasumulu wilayani Kyela, ulipo mpaka wa Tanzania na Malawi.

Hata hivyo, alisema jeshi hilo linaendelea kufanya mahojiano na dereva huyo ili kubaini mtandao mzima wa biashara haramu ya kusafirisha binadamu.

Kamanda Ngowi alisema wahamiaji hao walikutwa wakiwa na hali mbaya kiafya kutokana na kusafiri umbali mrefu bila kula pamoja na kuhifadhiwa kwenye gari ambalo halina dirisha wala mlango uliokuwa wazi kuruhusu hewa kuingia.

Aliwataka madereva kuacha kuwasafirisha wahamiaji haramu, huku akiwataka wamiliki wa magari kutoruhusu magari yao kutumika kwa shughuli hiyo kwa kuwa ni kinyume na sheria na adhabu yake ni kulipa faini, kwenda jela na magari yanayotumika kutaifishwa.

Inadaiwa kuwa wahamiaji hao walikuwa wanajisaidia ndani ya gari hilo na kubabisha harufu mbaya baada ya mlango kufunguliwa.

Wimbi la wahamiaji haramu raia wa Ethiopia kukamatwa mkoani Mbeya limeshamiri, Oktoba 22, mwaka jana, walikamatwa 22 wilayani Mbarali na wengine 57 walikamatwa Desemba 15, wilayani Rungwe.

# Dola mil. 425 kuboresha elimu ya juu

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB), inatarajia kutumia zaidi ya Dola za Marekani 425 kutekeleza mradi wa kuboresha elimu ya juu ya mabadiliko ya kiuchumi (HEET).

Akizungumza jana wakati wa ufunguzi wa kikao cha wadau kujadili rasimu ya miongozo ya usalama wa mazingira na jamii katika utekelezaji wa mradi wa kuboresha elimu ya juu ya mabadiliko ya kiuchumi (HEET) kwa wanufaika wa moja kwa moja wa taasisi za serikali, Katibu Mkuu, Dk. Leonard Akwilapo, alisema mradi huo ni muhimu kwa kuwa utaleta mabadiliko makubwa ya kitaaluma nchini.

Alisema kikao kingine cha wadau kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali kitafanyika leo lengo ni kupata maoni ya wadau katika maboresha na utekelezaji wa miradi huo na wanataaluma, na kesho kutakuwa na kikao cha wadau wengine.

Kwa mujibu wa Dk. Akwilapo, mradi huo unakuja kujibu changamoto za elimu zilizopo nchini na kuishukuru WB kwa kufadhili mradi unaotambua mahitaji ya nchi katika sekta ya elimu.

"Yatakayofanyika ni mageuzi maboresho ya mfumo wa elimu ya juu ili kuwe na mabadiliko chanya katika nyanja zote za kukuza uchumi wa nchi. Na ili kufanikiwa ni lazima kuwe na ushiriki wa wadau wote muhimu kwa masuala ya elimu ya juu," alisema.

Katibu mkuu huyo alisema kuwa mradi huo utaongeza rasilimali watu, wahadhiri, maabara, wakutubi, kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, kuhuisha mitaala na kuanzisha programu mpya ili kuwezesha watu kujiajiri au kuajiriwa, kuongeza udahili wa wanafunzi ikiwamo wa kutoka nje ya nchi.

Vile vile, mradi huo utaimarisha mfumo wa malezi chuoni kwa kuwapa elimu inayowafanya wajitambue kama Watanzania na kwamba wanataaluma 639 wa ngazi ya shahada za umahiri na udhamiri watasomeshwa ili kuongeza idadi yao katika nyuo vikuu nchini.

"Mradi utaboresha au kuanzisha mitaala na programu 290 zitakazoendana na soko la ajira, kukarabati miundombinu katika vyuo 15 vya umma, na taaisisi nne za wizara, kununua vifaa vya kisasa vya TEHAMA na mafunzo kazini ili kupata mbinu za kisasa za ufundishaji," alibainisha.

Dk. Akwilapo alisema udahili wanafunzi kwa sasa ni zadi 90,000 na miaka mitatu ijayo watafikia zaidi ya 180,000 na kwamba mradi huo umekuja kwa wakati muafaka kwa kuwa utakidhi mahitaji yote muhimu.

"Licha ya kuongeza idadi ni lazima ubora wa elimu kuwa wa hali ya juu, kuwe na walimu wanaoendana na idadi ya madarasa, wanafunzi na vifaa vilivyopo ili kuhakikisha kiwango cha elimu inayotolewa ni bora. Mafanikio yatapatikana kama kutakuwa na umakini, mradi utekelezwe kwa kiwango cha juu," alisema.

Awali, Naibu Katibu Mkuu Sayansi, Prof. James Mdoe, alisema maoni ya wadau yatasaidia kuboresha baadhi ya maandiko kwa ajili ya mradi wa elimu ya juu wa mageuzi ya kiuchumi na kwamba wizara imepewa malengo ya kuelimisha nguvu kazi kwa ajili ya ujenzi wa uchumi na katika kutekeleza inahitaji rasilimali fedha na watu.

PASS
PRIVATE AGRICULTURAL SECTOR SUPPORT

APPOINTMENT



Ms. Anna Shanalingigwa
Acting Managing Director PASS Trust

The Board of Trustees of The Private Agriculture Sector Support Trust (PASS) is pleased to announce the appointment of Ms. Anna Shanalingigwa as the Acting Managing Director of the Trust effective 1st January 2021. Ms. Shanalingigwa has been the Chief Operations Officer of the Trust and possesses an impeccable performance record from various national and international organizations that she had served in the past.

As The Board, we congratulate Ms. Shanalingigwa as she assumes this leadership role of the PASS Team.

**Prof. Andrew E. Temu**
**Chairman of The Board of Trustees**

"Improving quality of life through agribusiness transformation"

@passtrust pass@pass.or.tz www.pass.or.tz

# TAKUKURU yaokoa nyumba 2 ikiwamo ya mwanariadha

**Na Thobias Mwanakatwe**

TAASISI ya Kupambana na Kuzuia Rushwa Nchini (TAKUKURU), Mkoa wa Songwe imefanikiwa kurejesha Sh. 17,841,600 pamoja na nyumba mbili, ikiwamo ya aliyekuwa bingwa wa taifa wa mbio fupi nchini miaka ya 1980, Nzael Kyomo, anayeishi nchini Marekani.

Akitoa taarifa ya utekelezaji kwa waandishi wa habari jana, Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, Dk. Damas Sutta, alisema walifanikiwa kurejesha fedha na nyumba hizo baada ya kupokea malalamiko na kuyafanyia kazi.

Alisema kiasi hicho cha fedha kiliokolewa kutoka kwa kampuni, watu binafsi, pamoja na watumishi wa umma ambao hufanya kazi zao bila kuzingatia sheria na kanuni za nchi.

Alitaja sehemu ya fedha zilizookolewa kuwa ni za kampuni ya kuuza mbegu, Highland Seeds ya jijini Mbeya, Sh. 4,491,600 kutoka kwa wananchi waliokopa mbegu.

Alisema fedha nyingine zilizookolewa ni Sh. 1,200,000 ambazo mkazi wa Mtaa wa Ilembo, wilayani Mbozi, Emiliana Sakimela, alimkopea Kaimu Ofisa Mtendaji wa Mtaa Ilolo, Rehema Mwandulusya, kutoka kwa watu mbalimbali na kugoma kurejesha.

Akizungumzia kuhusu nyumba zilizookolewa, Dk. Sutta alisema TAKUKURU ilifanikiwa kurejesha nyumba hizo baada ya kupokea malalamiko na kufanya uchunguzi na kubaini ukweli kabla ya kuzirejesha kwa wahusika.

"Mfano huyu mwanariadha wa zamani ndugu Nzael Kyomo, yeye nyumba yake ilidhulumiwa na mtoto wa dada yake aliyemlea mwenyewe na aliamua kujibinafsisha nyumba hiyo baada ya kuona mama huyo mdogo hakuwa hapa nchini kwa muda mrefu."

Alisema Kyomo alidhulumiwa nyumba yake iliyopo Mji wa Mlowo, wilayani Mbozi na Emmanuel Mkondya, ambaye ni mtoto wa mdogo wake ambaye alikaribishwa kwa ajili ya kumsaidia mama mzazi wa mwanariadha huyo.

Alisema TAKUKURU pia ilifanikiwa kurejesha nyumba nyingine katika mji huo, ya Edmond Masebo, iliyokuwa imechukuliwa na Edward Kalonge, kutokana na mkopo umiza wa Sh. milioni 30.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Blasius Chatanda, akizungumza na waandishi wa habari mkoani humo jana, baada ya jeshi hilo kukamata gari la kubebea maiti likiwa limebeba dawa za kulevya aina ya mirungi. **PICHA: BONIFACE GIDEON**


NHC

## TAARIFA KWA WAPANGAJI WA NYUMBA ZA NHC WANAODAIWA KODI NA MALIMBIKIZO

1. Shirika la Nyumba la Taifa linawashukuru wapangaji wake walioweza kulipa kodi na malimbikizo yao baada ya kupewa notisi ya siku kumi na nne (14) ya kulipa kodi na malimbikizo wanayodaiwa. Aidha, wapo wapangaji wachache ambao bado wanadaiwa kodi na malimbikizo hadi sasa.
2. Kwa mara nyingine, Shirika linatoa siku thelathini(30) kwa wapangaji wanaodaiwa kodi na malimbikizo kufika katika ofisi za Shirika zilizo karibu nao ili kulipa kodi na malimbikizo wanayodaiwa.
3. Shirika linawashauri wapangaji wote kutumia fursa hii kulipa madeni yao na baada ya muda huu uliowekwa kukamilika, Shirika litatumia taratibu za kisheria kukusanya kodi na malimbikizo yanayodaiwa wapangaji ikiwemo kukamata na kupiga mnada mali za wapangaji ili kufidia kodi na malimbikizo yanayodaiwa. Aidha, baada ya muda huu kupita, Shirika halitasita kutangaza kwenye vyombo vya habari majina ya wadaiwa wote sugu ili umma ufahamu watu wanaokwamisha maendeleo ya Shirika na Taifa kwa kutokulipa kodi.
4. Tunashukuru wapangaji wote wanaotimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa wakati na kuliwezesha Shirika na Taifa kuwaletea maendeleo watanzania kwenye sekta ya nyumba.

**IMETOLEWA NA: OFISI YA MAWASILIANO NA HUDUMA KWA JAMII**
**NHC-MAKAO MAKUU**

SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
MAKAO MAKUU S.L.P 2977 | DAR ES SALAAM TANZANIA
| SIMU: +255 22 2105001-5 | NUKUSHI: +255 22 2105000
BARUA PEPE: dg@nhctz.com | TOVUTI: www.nhctz.com


# Wafanyabiashara wanaoficha mafuta Kahama waonywa

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama, mkoani Shinyanga imewaonya wafanyabiashara wa mafuta ya kula wanaoficha bidhaa hiyo na kuwataka wayatoe katika maghala yao na kuyauza kwa wananchi.

Kukosekana kwa bidhaa hiyo katika maeneo mbalimbali kumesababisha kupanda kwa bei na kukosekana katika maduka yaliopo katika maeneo hususani katika Halmashauri ya Mji wa Kahama.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alitoa onyo hilo juzi wakati akiongea na mwandishi wa habari hizi.

Macha alisema bei ya mafuta katika Wilaya ya Kahama imepanda kwa kiasi kikubwa na kwamba wapo baadhi ya wafanyabiashara wametumia mwanya huo kuficha bidhaa hiyo na kuleta ugumu kwa walaji wa mji huo.

Alisema baadhi ya viwanda vya mafuta katika maeneo mbalimbali vimekosa uzalishaji kutokana na kukosa malighafi ambayo ni mbegu, huku akisisitiza wakulima kulima mazao ambayo yatakuwa yakitoa bidhaa hiyo kupitia mbegu zake kama alizeti na pamba.

Mkuu huyo wa wilaya ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kahama, alisema hali bidhaa hiyo si nzuri na kuongea kuwa watu wanapata tabu kutokana na bei iliyopo kwa sasa ambayo ni wastani wa Sh. 80,000 kwa lita 20.

Alisema, serikali imesema kuwa mafuta yameanza kuingia kwa wingi kutoka nje na watu hawana budi kuyachangamkia kuyatumia na kuwataka wafanyabiashara kuacha kuficha bidhaa zilizopo kutokana na kukosekana sokoni kwa ajili ya kupandisha bei kwa wananchi.

Alisema kufanya hivyo ni kuwaumiza wananchi wenye kipato cha chini kwa kuwa walio wengi wanatumia bidhaa hiyo na kuwaomba kuyatoa na kuanza kuyauza kwa watu waweze kukidhi mahitaji yao katika familia pamoja na biashara zinazohitaji mafuta hayo. Macha alisema, kwa sasa kuna mazao mengine mapya yanakuja katika msimu ujao wa kilimo na kuongeza kuwa ni bora kwa wafanyabiashara kutumia muda uliopo kuuza bidhaa zilizopo ndani ili zisije zikakutana na za msimu uliopita.

"Tunawaomba wafanyabiashara wasifiche mazao yao kwa nia ya kusubiri yapande bei katika msimu ujao wa kilimo kwani yatakutana na yale mazao mapya na hivyo kufanya uuzwaji wake kuwa mgumu kutokana na wingi wake kwa wakati huo," aliongeza.

# Mgomo wa daladala watikisa Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MADEREVA daladala jijini Dodoma, jana waligoma kutoa huduma ya usafiri kwa abiria kwa saa kadhaa, wakishinikiza kufanyiwa ukarabati eneo la stendi ya Sabasaba.

Wakizungumza na waandishi wa habari, baadhi ya madereva walidai eneo hilo halijafanyiwa ukarabati licha ya kulilalamikia kwa muda mrefu, huku wakiendelea kulipa ushuru kila siku.

Mmoja wa madereva hao, Ayoub Mazengo, alisema licha ya wao kulipa ushuru kila siku kwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, miundombinu ya stendi hiyo ni mibovu.

Alisema pamoja na kutofanyiwa ukarabati, kero nyingine ni eneo hilo kuwa dogo, kushindwa kukidhi idadi ya daladala.

"Tumekuwa tukitoa ushuru kila siku, lakini hakuna kinachofanyika na hivi sasa msimu wa mvua eneo linakuwa shida kupitika kutokana na tope na mashimo yanayotokana na mvua, lakini eneo hili ni dogo na kuna wafanyabiasahra wengine wanalitumia," alisema Mazengo.

Alisema pamoja na eneo hilo kutokuwa na miundombinu rafiki pia kitendo cha wafanyabiashara wengine wa mboga na matunda kulitumia imekuwa usumbufu kwao.

"Pamoja na wafanyabiashara hawa wa mboga na matunda, wako watu ambao wanafanya biashara ya kuchoma mahindi na mishkaki wanaotumia majiko ya moto ambayo ni hatari kwa magari kwani yanaweza kulipuka moto na kuleta maafa," alisema.

Pia, alisema wamekubaliana kutoingiza gari lolote katika stendi hiyo hadi hapo itakapofanyiwa ukarabati au kufanyika kwa makubaliano mengine yatakayokuwa yanazingatia matakwa yao na si vinginevyo.

Naye Abdul Mohamed alisema jiji bado halijawahakikishia kuwa eneo hilo ni kwa ajili ya stendi au soko, lakini wamekuwa wakitozwa ushuru wa Sh. 1,000 kwa takribani magari 2,000 ambapo kwa siku sawa na Sh. milioni tatu.

"Lakini wanashindwa kututengenezea miundombinu hapa unaona matope yamejaa, lakini magari yanavunja 'spring'. Tunashindwa kugeuza tunavunjiana taa za magari, lakini mbaya zaidi tunajikuta tunalipa nyanya au mikokoteni ya wafanyabiashara ambao pia wako ndani ya stendi," alisema.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, akitolea ufafanuzi malalamiko ya madereva hao, aliomba muda wa siku 10 ili kumalizia ukarabati wa stendi ya Makole na Majengo ili kuhamisha baadhi ya magari.

Alisema hivi sasa stendi inayotumika ya Sabasaba ni ndogo kulinganisha na idadi kubwa ya magari yaliyopo.

# Kamati za Bunge kukutana Jan. 18

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI za Kudumu za Bunge la 12, zinatarajiwa kuanza vikao vyake wiki ijayo huku miongoni mwa shughuli zitakazofanyika ni pamoja na uchaguzi wa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, Ofisi ya Bunge, kamati hizo zitakutana kutekeleza majukumu ya kibunge kuanzia Januari 18 hadi 31, mwaka huu, kabla ya kuanza mkutano wa pili wa Bunge Februari 2, mwaka huu.

Ilieleza kuwa kamati hizo zitaanza kwa kufanya uchaguzi wa wenyeviti na makamu wenyeviti wa kamati zote.

Pia kwa muda huo kutakuwapo na mafunzo kwenye kamati mbalimbali ikiwamo ya majukumu na taratibu za uendeshaji wa kila kamati.

Mafunzo mengine ni kuhusu Bunge mtandao na usalama wa mtandao kwa kamati zote, kamati za kisekta kupokea maelekezo ya wizara kuhusu muundo, majukumu ya taasisi pamoja na sera na sheria zinazosimamiwa na wizara hizo.

Vile vile, kutakuwa na mafunzo kwa Kamati za Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC) na Kamati ya Bajeti kuhusu uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Msajili wa Hazina (TR) na namna bora ya kuhoji Maofisa Masuuli.

Kadhalika, kutakuwapo na mafunzo kwa Kamati ya Sheria ndogo kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo na uzoefu wa mabunge mengine ya nchi zinazofuata mfumo wa kibunge wa Jumuiya ya Madola.

Katika taarifa hiyo, ilibainisha majukumu matano ya Kamati ya Bajeti katika kipindi hicho ikiwamo kupokea na kujadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka miaka mitano kuanzia 2021/22 hadi 2025/26.

Majukumu mengine ya kamati hiyo ni kupokea na kujadili taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa miaka mitano 2016/17 hadi 2020/21.

Pia kupokea na kujadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka mmoja 2021/22, mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22 na taarifa ya utekelezaji wa bajeti pamoja na Sheria ya Fedha kwa kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2020/21.


**Bank of India (Tanzania) Ltd.**

*Relationships beyond banking*

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA

**DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019**

**MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)**

| NO. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE | |
|---|---|---|---|
| | | USD | TSHS |
| 1.0 | **Current Accounts** | | |
| a) | Required minimum opening balance | 500 | 500,000 |
| b) | **Monthly service fee (breakdown per customer)** | | |
| | Folio Charge | 4 | 6,000 |
| c) | Cheque withdrawal over the counter | | |
| | Up to Tshs 25,000,000 a day | - | free |
| | Over 25,000,000 a day | - | 0.15% of withdrawn amount |
| | Up to 5000 USD a day | free | - |
| | Over 5000 USD withdrawal | 0.6% of withdrawn amount | - |
| d) | Fees per ATM withdrawal | - | - |
| e) | ATM mini statement | - | - |
| f) | Interim/additional statement per page | 1.50 | 1500 |
| g) | Periodic scheduled statement | free | free |
| h) | Cheque book **(50 leaves)** | 27 | 42,000 |
| i) | Dishonoured Cheque | 55 | 70,000 |
| j) | Special clearance | | |
| | Within walking distance 1km | 45 | 70,000 |
| | More than 1km | 65 | 95,000 |
| k) | Counter cheque | - | - |
| l) | Inward/Outward cheque collection-USD | 0.60% Min comm. 18 postages USD 90 | - |
| m) | Cancelation of bankers cheque/DD | 15 | 20,000 |
| n) | | | |
| o) | Stop payment | 28 | 35,000 |
| p) | Standing order | - | - |
| q) | Balance enquiry | free | Free |
| r) | Issue of Balance certificate | 7 | 9,000 |
| s) | New ATM card issuance | - | - |
| t) | ATM card renewal or replacement | - | - |
| u) | Overdrawn account interest charge | - | - |
| | Overdrawn in current account | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| | Overdrawn in loan account | 2% over regular rate | 2% over regular rate |
| | Unarranged overdraft | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| v) | Interbank transfer | - | - |
| w) | Bill payments through ATM | - | - |
| x) | Deposit fee | - | - |
| | **Savings Accounts** | | - |
| | (Up to USD 5000) | Free | - |
| | (Over USD 5000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency | - |
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| v) | Other (please specify) | | |
| | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | |
| | | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| v) | Other (please specify) | | |
| | | | |
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| v) | Other (please specify) | | |
| | | | |
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| v) | Other (please specify) | | |
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| v) | Other (please specify) | | |
| | | | |
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| v) | Other (please specify) | | |
| | | | |
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| v) | Other (please specify) | | |
| | | | |
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| | Cheque book charges 50 leaves | 27 | 42000 |
| | Account closure charges | 70 | 85,000 |
| | **Maintenance of minimum account balance** | 500 | 500,000 |
| | **Minimum balance charges** | 15 p.m | 20,000 p.m |
| **4.0** | **Electronic Banking** | | |
| a) | Internet banking monthly fee | - | - |
| b) | Internet transfers | - | - |
| c) | SMS banking | - | - |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

| | | Minimum SMS Alert Charge ( to be recovered quarterly upfront) | Number of Free SMS on paying SMS Alert charge | SMS Alert charge per SMS beyond the free SMS (To be recovered in monthly basis) |
|---|---|---|---|---|
| d) | SMS Alert facility - | | | |
| | - Individual | USD 3.00 (USD a/c) TZS 5,000 (TZS a/c) | 1st 50 SMS in a Qtr | USD 0.05 per SMS TZS 100 per SMS |
| | - Corporate | USD 10.00 (USD a/c) TZS 15,000 (TZS a/c) | 1st 150 SMS in a Qtr | USD 0.05 per SMS TZS 100 per SMS |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| e) | Others | - | | - |
| **5.0** | **Foreign Exchange Transaction.** | - | | - |
| a) | Purchase/sale of TCs transactions over the counter | - | | - |
| b) | Purchase of foreign Cheque. | - | | - |
| c) | Sale/purchase of cash passport. | - | | - |
| d) | Telegraphic transfer. | | | |
| | Remittances Outward(TISS) | 10 | | 10,000 |
| | Other Outward remittances: | | | |
| | | A/C holder | Non A/C holder | |
| | Up to USD 6,000 | 15 | 40 | -- |
| | USD 6001-10,000 | 30 | | -- |
| | Above USD 10,000 | 0.35%max USD 210 | | -- |
| e) | Telex/SWIFT. | 30 | | - |

| | | | |
|---|---|---|---|
| f) | Transfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank). | | |
| **6.0** | **Other Charges** | | |
| a) | Activation of Dormant Accounts - Per Activation | | |
| | - Individuals | 3 | 5,000 |
| | - Corporate | 6 | 12,000 |
| **7.0** | **Personal Loans. Charges** | | |
| a) | Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| i) | Personal loans | 1.50% | 1.50% |
| ii) | Overdrafts | 1.50% | 1.50% |
| iii) | Mortgage finance | 1.50% | 1.50% |
| iv) | Asset finance | 1.50% | 1.50% |
| b) | Unpaid loan instalment | 5.00% Over the applicable rate | |
| c) | Early repayment | 2.5% of prepaid loan amount | |
| d) | Valuation fees | As per actual charges by valuer | |
| e) | **Others** | | |
| i) | Documentation charges | Actuals as per advocate bill | |
| ii) | Document Handling Charges | 0.30% of loan amount | |
| iii) | Inspection Charges | Tshs 30,000 per visit | |
| iv) | Modification charges | 0.25% on the sanctioned limit | |
| **8.0** | **Guarantee (Performance/Financial)** | | |
| | Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part there of minimum for one quarter | |
| | Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| **9.0** | **Imports** | | |
| | LC opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| | LC amendment charges | Per amendment 0.40% of LC mount (minimum USD 60 and maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (same for LC against 100% cash margin) | |
| | Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 180 | |
| | Retirement of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Inward Bills for collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 | |
| **10.0** | **Exports** | | |
| | Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC advising charges | USD 150 | |
| | Export Bills for collection | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | | | |

No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the period covered by the disclosure

No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the period covered by the disclosure

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ashwani Kumar Negi | Managing Director | Signed | 07.01. 2021 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | Head of Finance | Signed | 07.01. 2021! |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 01.01. 2021! |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wananchi zingatieni utabiri wa hali ya hewa

**MVUA** inayoendelea kunyesha katika maeneo mengi nchini ni utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), uliotolewa mwishoni mwa wiki wa kuwapo kwa mvua kubwa itakayoambatana na upepo.

Utabiri huo ni kutoa tahadhari kwa wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathirika na mvua hasa ya mabondeni.

Mvua inaponyesha tumeshuhudia maeneo mengi yakiathirika kwa mafuriko licha ya mabondeni, lakini kwenye barabara za mijini.

Mafuriko husababishwa na mambo mengi ikiwamo uchafu unaotupwa kwenye mifereji ya kupitisha maji barabarani na watu wasiokuwa na chembe ya aibu ya kugeuza mitaro hiyo kuwa madampo hali inayosababisha kuziba na maji kushindwa kupita.

Pamoja na TMA kutahadharisha watu kuhama maeneo yenye hatari ya kukumbwa na mafuriko, lakini baadhi huwa wakaidi kwa kudai kuwa maji yatapita na wao maisha yataendelea kama kawaida bila kujali athari inayowakumba.

Tumeshuhudia watu kukosa makazi baada ya nyumba zao kuzingirwa na maji, samani za ndani, vyakula kusombwa na maji na uharibifu mkubwa unaosababishwa na mafuriko hayo.

Vifo vingi pia vimeripotiwa katika maeneo ya mabondeni na waathirika wakubwa huwa ni watoto na watu wazima ambao hujaribu kuokoa maisha ya watoto hao.

Licha ya kutokea kwa athari hizo, lakini baadhi ya wananchi wameendelea kuwa sugu na kung'ang'ania kuishi kwenye maeneo hatarishi.

Wengine hutoa sababu kuwa nyumba wanazoishi wamezijenga kwa kudunduliza na hawana tena kipato cha kujenga sehemu nyingine.

Miaka ya nyuma kulitokea janga kubwa la mafuriko eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam, ambalo lilisababisha watu kupoteza maisha na nyumba kadhaa kubomoka na serikali iliamua kuwasaidia wakazi wake kwa kuwapa viwanja eneo la Mabwepande, wilayani Kinondoni, nje kidogo ya jiji.

Hata hivyo, baadhi ya watu waliopewa msaada huo ukiwano wa vifaa vya ujenzi waliamua kuuza na kurudi kule kule kwenye janga na kila linapotokea tatizo la mafuriko kilio kinarudi kwa serikali kuwaokoa na janga hilo.

Wananchi kuiomba serikali yao msaada ni jambo la kawaida, lakini kama ilishatoa tahadhari, kuwahamisha eneo la hatari na kuamua kurudi ni jambo la kufikirisha.

Serikali inatumia fedha nyingi kwenye majanga kama hayo kuokoa na kutoa msaada kwa wananchi wake ili kuwaweka salama.

Kuna helikopta zinatumika kufanya doria angani na kuokoa ambazo zinahitaji mafuta, kuna dawa zinahitajika kwa wanaokuwa kwenye hali mbaya kiafya na vyakula kwa waliopoteza kila kitu kwa kusombwa na mafuriko.

Kama wananchi wangezingatia tahadhari zinazotolewa, fedha hizo zingetumika kufanya maendeleo kwenye maeneo mengine.

Ni jukumu la kila mmoja kuzingatia tahadhari zinazotolewa na tunapotaka kuweka makazi lazima tufuate taratibu za mipango miji ili kuepuka madhara ambayo tunayashuhudia hivi sasa yanayosababishwa na mvua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kulikoni mvua tu, tunatupa taka, kuzibua vyoo kutiririsha majitaka

Na Yasmine Protace

**MVUA** inanyesha hivi sasa. Mengi yanasemwa ndani ya kipindi cha mvua. Wakulima wanafurahia uhalisia, maana nguvu ya jembe lao inamea.

Kwingine na hasa katika baadhi ya mitaa ya mijini penye 'mchanganyiko maalum' nako kuna yake, vyoo vinashiba na wenye kuvipa nafuu wanafanya kazi ya utiririshaji maji machafu.

Hata hivyo, bado kwa jumla mvua inaponyesha, watu hujawa na neema, kwa sababu wengine kupitia mvua hiyo hiyo, wanakinga maji ya kunywa na kupikia na hata kuogea, hivyo inamsaidia mtu huyo aliyetaka kununua maji, sasa hanunui tena.

Ni leo jijini Dar es Salaam, mvua hiyo ina mazito yake. Mtu akienda lililoko Soko la Vyakula la Mabibo, atakutana na makuu ya maji, ikiambatana na uchafu, pia lindi la matope kibao.

Mvua hiyo hiyo inakuwa imeanzisha ajira aina yake, kinamama wanajiongezea kipato kwa kufanya kazi mahali pa kuingia na kutoka sokoni, wakiwanawisha waliochafuka miguuni.

Ningependa kulizungumzia hilo kwa faida yetu na afya zetu na isiwe kero kwetu. Sasa hii inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilishadokeza mikoa mingi ingekabiliwa na mvua, ikiwamo Dar es Salaam.

Lingine tena la majitaka! Kupitia adha na usumbufu wa mvua na vyoo 'kushiba' majitaka, hali inakuwa mbaya kwa watumiaji, nao wanashindwa kuwa wazalendo. Hapo ndipo wanakuja na msamiati 'kuvitapisha' ambao vitendo vyake ni vibaya zaidi.

Ni vyema tuulizane, ni kweli inakuingia akilini kushindwa kulipia gari la kunyonya majitaka hizo na hata unafikia mbadala wa kuamau kutumia 'mateja' wakuzibulie choo na hicho kinachotiririka kinasambaa kwenye makazi ya watu.

> **Ni vyema tuulizane, ni kweli inakuingia akilini kushindwa kulipia gari la kunyonya majitaka hizo na hata unafikia mbadala wa kuamau kutumia 'mateja' wakuzibulie choo na hicho kinachotiririka kinasambaa kwenye makazi ya watu.**

Mtu anatoa uchafu wake unaoenda kwenye makazi ya watu, wakati hapo kuna watoto na biashara zinazoendelea.

Huko ni kukosa ustaarabu, mbadala ni kuharibu mazingira na afya ya majirani. Kwa kufahamika rasmi kuwapo mambo kama hayo, ndio maana kuna magari maalum ya kufanya kazi ya kunyonya majitaka.

Nikupe mfano, mtu akiwa katika maeneo kama Kariakoo jijini Dar es Salaam, atashangaa kuona maji ya harufu mbaya yanamwagika kwenye mazingira ya mitaa na ukihoji kulikoni, unajibiwa "wameishafungulia vyoo vyao."

Kufanya hivyo 'unatapisha' ujue pia unawasababishia wenzako jirani wawe wakazi wakubwa kwa watoto na wafanyabiashara wanaingizwa katika mfumo wa kuathirika na uchafu huo.

Staili nyingine, kuna wale ambao mvua zinaponyesha, basi ndio fursa yenye nafuu ya kutupa taka walishahifadhi ndani kupitia mitaro.

Jamani, serikali imeingia gharama kubwa kujenga mitaro hiyo isafirishe maji kutoka sehemu moja kwenda nyingine, lakini cha kushangaza miundombinu hiyo ndiyo nyenzo ya kutupa taka za kila aina na kuifanya inaziba.

Watu wanatakiwa kuwa wastaarabu, kwamba panapokuwapo umuhimu wa kutunze afya na mazingira, wawajibike kila mmoja kwa nafasi yake na sio kuharibu miundombinu hiyo.

Kwa sasa mtu akipita kwenye maeneo yenye mifereji, daima atakuta taka zinaelea kwenye mifereji hiyo iliyoziba.

Tukitafakari namna gharama zinavyoingiwa kuzibua mitaro kutokana na taka, kisha upande wa pili mtu anarahisisha kutupia taka, maana yake inakuwa nini?

Ukusanyaji na utupaji taka kila eneo una utaratibu wake rasmi na wa kisheria ambao haupaswi kugeukwa.

Mara nyingi unaendana na malipo maalum yanayofikiwa katika mipango na kanuni za kidemokrasia za halmashauri zao, zikitekelezwa na waidhinishaji wake ni wawakilishi rasmi, madiwani.

# Miti inayogeuka mawe yawavutia wageni wengi

**Na Gideoni Mwakanosya,** SONGEA

KIJIJI cha Mbati kilichoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, kina msitu wenye magogo yaliyogeuka mawe, hali inayovutia wageni mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi kukitembelea.

Mratibu wa Utalii Kanda ya Kusini na pia Ofisa Msaidizi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Wilaya ya Tunduru, Debora Hemily, alisema jana kuwa miti inayogeuka mawe (miti mawe) ni jamii ya miti ya mitetereka ambayo duniani inapatikana nchi mbili tu; Marekani na Tanzania.

"Kwa Tanzania miti mawe inapatikana Mkoa wa Ruvuma katika Kijiji cha Mbati, Wilaya ya Tunduru. Miti hiyo pia inapatikana katika Wilaya ya Namtumbo eneo la Likuyu, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na katika Pori la Akiba la Liparamba Wilaya ya Nyasa," alisema.

Alibainisha kuwa miti hiyo kabla ya kugeuka jiwe, inakuwa ni miti ya kawaida, lakini baada ya miaka kadhaa inageuka jiwe zito kutokana na mfumo wa asili ambao Mungu ameutengeneza.

Alisema kivutio hicho cha miti mawe kinaufanya utalii wa Mkoa wa Ruvuma kuwa ni wa kipekee na tofauti, akibainisha kuwa miti hiyo ina uwezo wa kudumu kwa zaidi ya miaka 120.

Hata hivyo, mtaalamu huyo wa uhifadhi, alisema miti hiyo ipo katika hatari kubwa ya kutoweka kutokana na watu wengi kuikata kwa matumizi mbalimbali, akisisitiza wananchi kuona haja ya kuihifadhi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Sandali Mtenje, mmoja wa wazee katika kijiji hicho, alisema aliona vipande vya mti uliogeuka mawe tangu mwaka 1983 na kwamba miaka hiyo vipande hivyo vya magogo vilikuwa katika hatua za awali za kugeuka mawe. Alibainisha kuwa miaka ya 1990, waliona wageni wengi wanatembelea mara kwa mara msitu wa kijiji hicho wakiwamo raia wa kigeni ambao walifika kuona miti hiyo ikiwa imegeuka mawe.

"Baada ya muda, tukagundua wazungu wanafika hapa tena bila hata kuona viongozi wa kijiji, wanabandua magamba ya miti hiyo na wengine wanachukua vipande vya miti iliyogeuka mawe na kuondoka navyo," alisema.

Utafiti uliofanywa katika Pori la Akiba Selous ambalo sasa limemegwa kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, umebaini kupatikana zaidi ya aina 2,100 za mimea zilizotambuliwa na wanasayansi zikiwamo aina 600 za miti ambayo haipatikani sehemu nyingine duniani.

Mkurugenzi mstaafu wa Uhifadhi ambaye amewahi kuwa Mkuu wa Chuo cha Wanyamapori Likuyuseka, Namtumbo, Ngwatura Ndunguru, anaitaja moja ya jamii ya miti ambayo haijafahamika na kutangazwa ipasavyo kuwa ni magogo ya miti iliyogeuka mawe jamii ya miti ya mitetereka ambayo kitaalamu inaitwa 'fossilized tree trucks'.

Anasema masalio ya magogo hayo bado yanaonekana katika baadhi ya maeneo ya ndani Hifadhi ya Selous (Hifadhi ya Taifa ya Nyerere) na katika vijiji vya Mpurakacheche na Mbarang'andu Wilaya ya Namtumbo, Mkoa wa Ruvuma.

Ngwatura anasisitiza kuwa miti mawe hiyo ikitangazwa kwenye vyombo vya habari, mamia ya watalii watakwenda Mkoa wa Ruvuma na kuona kivutio hicho kipya na cha kipekee, hivyo kuingiza mapato na fedha za kigeni ambazo zitasaidia kuinua uchumi wa nchi.

Ofisa Utalii wa Pori la Akiba Liparamba wilayani Nyasa, Maajabu Mbogo, alisema miti mawe inapatikana kwa wingi katika eneo la Nakatuta ndani ya hifadhi hiyo.

Kwa mujibu wa mhifadhi huyo, maeneo yote ambayo miti imegeuka mawe, hayakaliwi na watu wengi wala hakuna mtu anayeingia ndani ya eneo hilo, hivyo maeneo hayo yamebaki katika hali yake ya asili ya kiikolojia.



Gogo lililogeuka jiwe zito kwenye Msitu wa Mbogo wilayani Tunduru. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

## Baba wa kambo kortini madai kumbaka, kumpa ujauzito binti

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

MKAZI wa Kijiji cha Igunila, Kata ya Ziba, Igunga mkoani Tabora, Sharif Maganga (28), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Igunga kwa tuhuma za kumbaka binti mwenye umri wa miaka 14 na kumsababishia ujauzito.

Mwendesha Mashtaka wa Polisi Elimajid Kweyamba, alidai kuwa kijana huyo ambaye ni baba wa kambo wa binti huyo, alitenda kosa hilo kinyume na kifungu cha 130 (1) (2) (e) na 131 (1) cha Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 mapitio ya mwaka 2019 inayozuia kutenda makosa kama hayo.

Mbele ya Hakimu Mkazi, Eddah Kahindi, mwendesha mashtaka huyo alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya Januari na Agosti, 2020, mshtakiwa alikuwa akifanya mapenzi na binti huyo (jina limehifadhiwa) ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Igunila na kumsababishia ujauzito.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, mshtakiwa alikana na kesi hiyo imeahirishwa hadi Januari 19, mwaka huu, itakapotajwa na mshtakiwa amepelekwa mahabusu.

## Makandarasi wazawa wapigiwa chapuo

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi imeagiza Wakala wa Ujenzi wa Barabara (TANROADS), kutoa ajira ya miradi mikubwa kwa makandarasi wazawa ili waweze kujifunza na kupata ujuzi kutoka kwa wageni.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Leonard Chamuriho, alitoa agizo hilo baada ya kutembelea mradi wa ujenzi wa daraja la JPM na kukuta mtumishi mmoja pekee Mtanzania anayeendesha mtambo katika ujenzi huo na kutaka mikataba yote mikubwa iwekwe asilimia ya ushiriki wa moja kwa moja kwa makandarasi wazawa.

Alisema nchi inahitaji kuwa na makandarasi walio na ujuzi na weledi unaotokana na makandarasi wa kigeni ili wafanye kazi kubwa badala ya kufanya shughuli za kuchimba mchanga, kuvunja mawe ambazo ni kazi ndogo ndogo na zinazohusu teknolojia nzuri wageni ndio wanafanya. "Kampuni ya CCECC ipo nchini tangu mwaka 1967, lakini cha kushangaza hakuna mkandarasi aliyepata kujua kuendesha shughuli za ujenzi wa miradi mikubwa hapa Tanzania, jambo hili halikubaliki, hivyo naagiza miradi yote inayofuata katika kampuni hii nataka kuona kuna makandarasi wazawa waliopata mafunzo na ujuzi kutoka kwenye miradi inajengwa na hawa makandarasi wageni," alisema Chamuriho.

Aliagiza wananchi wanaozunguka mradi huo kupewa kipaumbele kwenye ajira, huku akitaka malighafi zinazopatikana katika Wilaya ya Misungwi, zianze kununuliwa ikiwa ni baada ya kuhakikiwa ubora.

Alisema wamekubaliana na wakurugenzi na viongozi kuwa ofisa uhusiano wa kampuni afanye utaratibu wa kuwatambua watu wanaohitaji ajira kupitia viongozi wa kijiji. "Tumeongea na Mkuu wa Wilaya (DC) wa Misungwi, Juma Sweda, naye ametoa changamoto zake, kuwa kuna malighafi aina ya benzonite yanatumika katika ujenzi wa daraja, lakini hayanunuliwi kwa wingi, tumekubaliana mkandarasi afanye utafiti wake kwa kushirikiana na Mhandisi Mshauri ili yanayopatikana kwenye maeneo ya Misungwi, yapimwe kwenye maabara zetu na TBS na wao kampuni itafute namna," alisema Chamuriho. Naye mhandisi mshauri wa mradi huo, Abdulkarim Majuto, alisema baadhi ya wataalamu waliokuwa wanatoka nje ya nchi na vifaa walishindwa kuwasili kwa wakati kutokana na corona na kusababisha kuchelewa kuanza mradi ambao ulianza Februari 24, 2020.

Daraja hilo la JPM lenye urefu wa mita 3.2 pamoja na barabara unganishi yenye urefu wa mita 1.66, linajengwa na kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) na China Railway 15 Group Corporation, kwa gharama ya Sh. bilioni 700.

## HABARI KITAIFA

## Washambuliwa na kujeruhiwa na fisi

**Na Marco Maduhu**, SHINYANGA

WATU wawili ambao ni wanafamilia, wakazi wa kijiji cha Kilimawe Wilaya ya Shinyanga, wamenusurika kifo kwa kushambuliwa na fisi, wakati wakiokoa kuku wao kuliwa na mnyama huyo.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Jumatatu majira ya saa 10:00 alifajiri, wakati wanafamilia hao walipoamka majira hayo na kwenda kuokoa kuku waliokuwa wamevamiwa na fisi kwenye banda.

Magiligimba aliwataja wanafamilia hao kuwa ni Mabuga Ndakuna (70) na mtoto wake Timotheo (17) ambao walishambuliwa sehemu mbalimbali za miili na kisha kupelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga kwa ajili ya matibabu.

"Mabuga Ndakuna aling'atwa na fisi huyo sehemu za kichwani upande wa kulia, na kuvunjwa mkono wa kushoto na kujeruhiwa pia mkono wa kulia, miguuni, mapajani na kwenye makalio. Bado anaendelea na matibabu na amelazwa," alisema.

"Timotheo Mabuga, yeye aling'atwa mkono wa kulia, paja na kushoto na alitibiwa kisha kuruhusiwa kurudi nyumbani, huku akiendelea kuuguza majeraha yake na anaendelea vizuri," aliongeza.

Kamanda Magiligimba alisema chanzo cha tukio hilo ni fisi kuvamia banda la kuku na wanafamilia hao kutoka nje kwenda kuwaokoa, ndipo wakaanza kushambuliwa na mnyama huyo.

Kutokana na shumbulio hilo, alisema wanafamilia hao walipata majeraha sehemu za miili yao na kubainisha juhudi za kuwaondoa wanyama hao wakali kwenye makazi ya watu zinaendelea kwa kushirikiana na maofisa wanyamapori.

# Wapinga Tunduru kuwa Halmashauri ya Mji

**Na Stevie chindiye,** TUNDURU

BAADHI ya wajumbe wamepinga mapendekezo ya kuipandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo Tunduru kuwa Halmashauri ya Mji kwa madai kuwa utaratibu huo ni kikwazo kwa wananchi.

Pia wamesema uamuzi huo utawafanya baadhi ya wananchi kusafiri zaidi ya kilometa 100 kufuata huduma za kijamii.

Uamuzi wa kupinga mji kupandishwa hadhi ulifanyika juzi wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) kilichofanyika kwenye Klasta ya Walimu Tarafa ya Mlingoti, mjini hapa.

Baadhi ya wajumbe walisema kitendo cha kupandishwa hadi mamlaka ya mji mdogo Tunduru kuwa halmashauri ya mji, hakiwatendei haki wananchi wanaoishi pembezoni hususani Jimbo la Tunduru Kusini.

Miongoni mwa wajumbe waliopinga pendekezo hilo ni Mbunge wa Tunduru Kusini, Daimu Mpakate, ambaye alisema vikao vilivyopita wakati vikijadili na kugawa Jimbo la Tunduru kuwa majimbo mawili, wajumbe walikubaliana kuwa ugawaji wa halmashauri zao uendane na mipaka ya majimbo hayo zikiwa ni juhudi za serikali kusogeza huduma kwa jamii.

Mpakate alifafanua kuwa pamoja na hoja hizo, pia uanzishwaji wa halmashauri hiyo bado haujakidhi vigezo vingi vikiwamo vya kuwa na idadi ya wananchi 150,000 na watatakiwa kuongeza kata tatu ambazo ziko umbali wa zaidi ya kilomita 35 nje ya eneo la mamlaka. Alisema hiyo ni tofauti na maelekezo yanayotaka kata za mamlaka kuwa ndani ya kilomita 15.

Awali, akiwasilisha taarifa ya mapendekezo hayo kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Gasper Balyomi, Ofisa Mipango wa Halmashuri, Jumanne Mwankoo, alisema tayari taratibu za ugawaji wa mipaka ya mamlaka yaa mji mdogo Tunduru zimekwishakamilika kwa kugawa na kuweka mipaka yake.

Alisema kwa mujibu wa maelekezo ya Tangazo la Serikali (GN) namba 353 la Septemba 17, 2004 mamlaka inaundwa na vijiji 32 vilivyoko katika Tarafa ya Mlingoti ambavyo vina kata 8 na kwa eneo hilo linakadiriwa kuwa na wananchi 72,874 wakiwamo wanaume 34,823 na wanawake 38,051.

Alisema matokeo ya idadi hiyo ya wakazi yametokana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 na kwamba malengo bado hayajafikiwa.

Mpakate katika taarifa hiyo, alimshangaa mkurugenzi kutaka kulitumia tangazo hilo la serikali kama fimbo ya kuwachapia wananchi wa maeneo ya vijijini na kuwafanya wapate taabu ya kwenda kufuata huduma umbali mrefu na kuongeza kuwa kama nia yake ni nzuri, mbona hakuzungumzia uanzishwaji wa mji mdogo wa Nalasi ambao pia ulitajwa kupitia tangazo hilo.

Hili ni pigo la tatu kwa mipango ya mkurugenzi kukataliwa kwa miradi mbalimbali iliyobuniwa na wataalamu wa halmashauri katika kipindi kifupi cha uongozi wa awamu ya tano ya kikindi cha pili na utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020- 25 .

Hivi karibuni madiwani na wabunge walikataa mradi wa ukarabati wa standi kuu ya mabasi yaendayo mikoani na kuikataa taarifa ya mapato na matumizi yaliyoidhinishwa na wataalamu wa halmashauri hiyo kipindi madiwani wakiwa katika mchakato ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.



Meya wa Manispaa ya Iringa, Ibrahimu Ngwada (kushoto) na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Himidi Njovu (kulia), wakishiriki ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi Chemchem, Iringa mjini juzi kama sehemu ya kuadhimisha miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Mganga mkuu asisitiza usafi kuepuka magonjwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Pwani, DK. Gunini Kamba, amesema endapo wananchi watazingatia usafi itasaidia kudhibiti magonjwa ya mlipuko ambayo yanaweza kusababisha kusimama shughuli za uzalishaji.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Dk. Kamba alisema kipindi cha ugonjwa wa corona kilisaidia hakuua magonjwa ya kipindupindu kwa kuwa wananchi walikuwa wanazingatia kunawa mikono mara kwa mara.

Dk. Kamba alisema njia mojawapo ya kujikinga na magonjwa ya maambukizi ni kunawa mikono mara kwa mara na usafi wa mazingira.

Alisema katika kipindi hiki cha mvua na msimu wa maembe, usafi unatakiwa kuwa wa hali ya juu, huku akisisitiza vyombo vya kunawia vilivyowekwa shuleni kipindi cha ugonjwa wa corona, viendelee kutumika kuwakinga watoto na magonjwa ya kuhara.

"Hiki kipindi cha maembe wanafunzi wasiposimamiwa katika suala la usafi inaweza kuwasababishia kupata ugonjwa wa kipindupindu kwani ni msimu wa maembe wataenda kuokota bila kuosha na kula uchafu," alisema.

Kuhusu suala la vyoo, Dk. Kamba alisema kila shule inatakiwa kuwa na vyoo vya kutosha ili wanafunzi wasiende kujisaidia porini ambako ni hatari kwao kupata magonjwa na hata kushambuliwa na wadudu na wanyama.

"Kusipokuwa na usafi ni hatari kupata magonjwa ya mlipuko kwa muda mrefu Pwani hatujapata ugonjwa wa kipindupindu na magonjwa ya kuhara yalisimama hasa kipindi cha COVID-19. Tunasisitiza wananchi waendelee na utaratibu wa kunawa mikono ili kudhibiti magonjwa haya yanayoepukika," alisema.

Dk. Kamba aliwataka wananchi kuwa makini na kwa atakayepata dalili za magonjwa ya mlipuko awahi kwenye kituo cha afya kupata matibabu ya haraka na ikiwezekana ajitenge ili kusiwe na maambukizi.

Alisema maofisa afya wa kata wanaendelea na utaratibu wa kutoa elimu ya usafi shuleni na mambo ya afya ili kuwawezesha wanafunzi kuepuka magonjwa na kujikinga na yale yanayoambukiza.

## Naibu Waziri ataka vitendo

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, ameitaka menejimenti na viongozi wa taasisi za sekta ya uchukuzi kufanya uamuzi ili kutochelewesha maendeleo kwa wananchi katika utekelezaji wa miradi.

Kasekenya alisema hayo juzi alipokuwa akifungua mkutano wa siku mbili wa Baraza la Wafanyakazi wa Sekta ya Uchukuzi lililofanyika mkoani Mwanza na kusema kuwa awamu hii imejikita katika matokeo na si mazoea.

"Katika awamu hii watendaji wengi wamekuwa wakichelewa kutoa maamuzi (uamuzi) katika maeneo mbalimbali sababu ya kutojiamini. Hii inafanya utekelezaji wa miradi kuchelewa kukamilika na kuchelewesha maendeleo kwa wananchi," alisema.

Mhandisi Kasekenya alitabaisha umuhimu wa kuwa na ratiba ya ukaguzi wa miradi kwa kila muhula na kusisitiza kuwa ukaguzi huo utawezesha kupunguza changamoto zinazojitokeza kwenye utekelezaji wa miradi.

Namna bora ya kutatua changamoto zinazojitokeza kwenye miradi ni kuwa na ratiba ya kukagua miradi hiyo mara kwa mara, na ratiba hizo zipangwe kwa miradi yote inayotekelezwa chini ya sekta," alisisitiza.

Pia alisema ni muhimu wataalamu wa sekta walio kwenye miradi kuchukua ujuzi wakati huu ambao miradi inaendelea ili utaalamu huo uwasaidie kusiimamia vizuri miradi itakapokamilika.

Naye Mwenyekiti wa Baraza na Kaimu Katibu Mkuu, Gabriel Migire, aliahidi kutekeleza maagizo hayo na kusisitiza kuwa kitengo cha ufuatiliaji na tathmini, uchukuzi kitaboresha kazi hiyo kuhakikisha inafanyika na kuleta matokeo chanya.

Baraza la Wafanyakazi la Sekta ya Uchukuzi, lilijumuisha menejementi na watumishi wa kila idara katika sekta na wakuu wa taasisi zilizo chini yake.

Pamoja na mambo mengine, baraza lilipitia utekelezaji wa miradi ya sekta na kuweka mikakati mbalimbali ya kuboresha utendaji.

# Wanaoficha watoto wenye ulemavu waonywa

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

SERIKALI mkoani Mtwara imewataka wazazi na walezi wenye watoto walio na ulemavu kuacha kuwaficha ndani badala yake watoe ushirikiano kwa serikali katika kuwabaini, ili kuwapatia misaada na kutimiziwa haki zao za msingi ikiwamo elimu na afya.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, alisema hayo juzi alipokuwa akizundua kampeni ya uchunguzi na ubainishaji wa watoto wenye mahitaji maalumu uliofanyika mkoani hapa katika Shule ya Msingi ya Majengo, Manispaa ya Mtwara Mikindani.

Byakanwa alisema kwanza anaishukuru Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kubuni mpango huo wa kuhakikisha watoto wote wenye mahitaji maalumu hasa wenye umri wa kwenda shule, wanapata elimu kama ilivyo kwa watoto ambao hawana ulemavu.

Alisema kuzinduliwa kwa kampeni hiyo mkoani Mtwara ni utekelezaji wa agizo la serikali la kutaka wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri kuanza kuwabaini watoto wenye mahitaji maalumu kwenye maeneo yao, ili serikali iwapatie misaada ya kimsingi ikiwamo elimu na misaada mingine ya kijamii.

Kwa mujibu wa Byakanwa, kila mtoto ana haki sawa, hivyo watoto wote wanatakiwa kupata haki zao za kimsingi kama vile elimu. Kwa sababu hiyo, alisema serikali mkoani Mtwara inatoa wito kwa wazazi na walezi kuacha kuwaficha ndani watoto wao wenye ulemavu badala yake wawafichue ili serikali iwabaini na kuwatambua kisha kuwapatia mahitaji maalumu.

Alisema wako watoto wenye ulemavu na wana uwezo mkubwa wa kufikiri na kwamba iwapo watapatiwa elimu, watakuwa msaada mkubwa kwa familia na kwa jamii lakini kutokana na wazazi kuwaficha ndani, wameshindwa kupata elimu, hivyo kuonekana kama si msaada jambo ambalo si sahihi.

"Kila mzazi mwenye mtoto ambaye ana ulemavu ashirikiane na serikali katika kufichua vitendo vya kuwaficha ndani badala yake wajitokeze kuwafichua ili serikali iwabaini na kuwapatia haki zao za msingi. Serikali mkoani hapa itahakikisha inawapatia haki zote watoto wenye ulemavu," alisema Byakanwa. Alisema kila wilaya na halmashauri za mkoa zitafanya kazi ya kuwabaini watoto wenye ulemavu na kuwaorodhesha ili kuwa na idadi maalumu na kuwaweka katika mpango utakaowawezesha kuwapatia mahitaji ya msingi. Ofisa Elimu Mkoa wa Mtwara, Kiduma Mageni, alisema kwa sasa mkoa wa Mtwara una vituo 22 vya elimu ya msingi vinavyotoa elimu kwa wanafunzi wa makundi maalumu na kwamba vituo hivyo viko katika halmashauri zote tisa za mkoa na vina uwezo wa kubeba wanafunzi 45,000.

Mageni alisema mpaka sasa mkoa una wanafunzi 858 wenye mahitaji maalumu wanaopata elimu na kati ya hao wavulana ni 457 na wasichana 401 na kusisitiza wazazi na walezi kuendelea kuwapeleka watoto kwenye shule hizo ili kupata elimu.

"Mkoa wetu unatarajia kuandikisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu 1,259 ndani ya mwaka huu na hiyo ni kwa halmashauri zote tisa zilizopo katika mkoa wa Mtwara na tuna matumaini makubwa ya kufikia lengo hili," alisema.



Wanafunzi wakitembea kwa miguu kuelekea shuleni umbali wa kilometa mbili katika eneo la Goba Tegeta A, jijini Dar es Salaam jana, kutokana na eneo hilo kukosa usafiri wa daladala kwa sababu ya ubovu wa barabara. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Maofisa ugani watakiwa kuelimisha wananchi kilimo kuepuka umaskini

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

MAOFISA ugani wametakiwa kutoa elimu ya kilimo bora cha mazao ya biashara kwa kaya zote maskini nchini zinazonufaika na ruzuku inayotolewa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini.

Kwa kufanya hivyo, imeelezwa kuwa kaya hizo zitapata kupata mavuno bora yatakayoziwezesha kuboresha maisha yao na kuondokana na umaskini.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, alitoa maagizo hayo juzi kwa maofisa ugani wa kijiji cha Mtinko wilayani Singida katika ziara yake ya kikazi iliyolenga kukagua utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini mkoani Singida.

Ndejembi amewahimiza wakurugenzi wa halmashauri na maofisa ugani wa halmashauri zote kutoa maelekezo kwa kaya maskini juu ya namna bora ya kulima mazao yanayostahimili ukame na kuendana na mazingira halisi ya maeneo husika ili kaya maskini zinufaike na kilimo.

"Maofisa ugani katika ngazi ya kata na vijiji waanze kuzitembelea kaya maskini na kuzisaidia namna ya kulima kitaalamu, ili kupata mavuno ya kutosha. Maofisa ugani waache kwenda kwenye miradi ya nyama pekee ambayo inawanufaisha kwa kujipatia fedha," alisisitiza.

Sambamba na hilo, Ndejembi alipokea shuhuda mbalimbali za mafanikio waliyoyapata wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini katika kijiji cha Mtinko.

Mmoja wa wanufaika, Leah Shila, alisema ameitumia fedha ya ruzuku aliyoipokea kujiwekea akiba kidogo kidogo na hatimaye kupata mtaji wa Sh. 200,000 uliomwezesha kufungua mgahawa.

Shila alisema kabla ya kuwa mnufaika wa TASAF, alikuwa akiishi maisha magumu yaliyomsababishia kula mlo mmoja kwa siku, lakini hivi sasa anakula milo mitatu na anasomesha watoto wake katika shule za msingi na sekondari.

Naye Zena Igwe alisema ametumia vizuri ruzuku aliyoipokea toka TASAF kwa kujenga nyumba bora ya kudumu kutokana na kuwekeza fedha kidogo kidogo ambazo zilimwezesha kununua saruji na mabati.

Aliongeza kuwa fedha hizo zimemsaidia pia kuanza shughuli ya ufugaji wa kuku ambao wamefikia 30 na anajishughulisha na kilimo cha bustani pamoja na kumsomesha mtoto wake elimu ya sekondari. Ndenjembi aliridhishwa na mafanikio hayo ya wanufaika wa TASAF na kuwataka wanufaika wote wa mpango huo kuzitumia vyema fedha za ruzuku katika shughuli mbalimbali za kiuchumi zitakazoboresha maisha yao na kuondokana na umaskini.

ama

ALHAMISI JANUARI 14, 2021

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Kinachofanikisha wenyeji wa Kagera wasisukumwe kusaka chanjo watoto**



Ukurasa 13

**MGANGA MKUU WA SERIKALI:**

**Sasa kazi, tuone vitendo kila mmoja akiwajibikia wagonjwa**

# LATRA: Tunatamani tusahau ajali kupitia vidhibiti mwendo kila basi

## •Kasi, mbwembwe njiani, uegeshaji ovyo

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), linasema watu 3,400 wanapoteza maisha kila siku duniani kupitia ajali za barabarani, huku dira ya ripoti yake ya usalama barabarani kuanzia 2011 hadi mwaka jana, iliangaza kufuta nusu ya ajali, majeruhi na vifo.

Ni tatizo linalogusa maisha ya watu hata kitaifa, mfano hai ikirejewa kauli za mwanzo za Inspekta Jenerali wa Polisi Mstaafu, Said Mwema, aliwahi kueleza hatua ya mafanikio kudhibiti uhalifu katika siku zake za mwanzo, lakini akikiri kutiwa ukakasi wa kusumbuliwa na usalama barabarani.

Kimsingi, usalama wa barabarani ni suala mtambuka lisiloishia mkononi mwa polisi pekee, bali linagusa mamlaka zingine za kiserikali na zisizo za kiserikali zinazosimamia usalama huo, kuanzia sheria hadi utendaji, abiria, madereva na watumia barabara.

WHO inaitaja ajali kuwa jambo linalowaacha pia waathirika katika ulemavu wa kudumu kimaisha na kuathiri mustakabali wa familia nyingi duniani, huku vifo hivyo vya ghafla vikiacha makovu ya kudumu kwa familia.

Inazitaja athari hizo ni kuwaacha majeruhi kila kona ya dunia na inaongeza mamilioni wanaosalia kuwa tegemezi wa kudumu katika baadhi ya mambo, kutokana na athari hizo.



Picha kuhusu yanayojiri barabarani na kelele za vidhibiti mwendo. **PICHA: MTANDAO.**

Kinachofanywa na WHO ni sehemu ya kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's), mahususi Namba Tatu, linalohusu afya na ustawi wa watu kwa rika zote ifikapo 2030.

Ni lengo linalohusu ambalo katika mustakabali wake mpana, unaangukia kupunguza vifo vya mama wajawazito, pia watoto wanaozaliwa.

Kuna hatua mbalimbali ambazo serikali na wadau zimeshachukua katika tafsiri na lengo la ama kupunguza au kumalizika kabisa nchini.

Hapo inajumuisha ushuhuda kama vile kuweka mfumo wa kisatelaiti wa kufuatilia mwenendo wa magari barabarani uitwao 'Vehicle Tracking System' (VTS), ambao unaofanana na mifumo iliyopo kwenye magari.

### VIDHIBITI MWENDO

Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri wa Barabara (LATRA), Johansen Kahatano, anasema hadi kufika mwishoni mwa mwaka jana, takribani mabasi 5,000 ya safari ndefu kivuka mikoa na mipaka ya nchi, yalifungiwa mfumo huo.

Kahatano anasema, licha ya kuendelea kuwapo matukio ya ajali barabarani, kwa kiasi kikubwa mfumo huo umepunguza ajali zilizosababisha vifo na majeruhi wengi nchini.

"Kufungwa mfumo huo kwenye baadhi ya mabasi, malalamiko ya abiria kuhusu madereva kuendesha vibaya yamepungua na hayajitokezi sana kama zamani," anasema Kahatano.

Pia, anafafanua kuwa ni mfumo unaorahisishia ufuatiliaji, kupata taarifa sahihi na za haraka, zitokanazo na mwenendo wa madereva kila kona ya nchi.

"Wito wangu ni kwa baadhi ya wamiliki wa mabasi wote wabadilike ili tusaidiane katika vita hii ya kudhibiti ajali, wahakikishe madereva hawachezei mfumo huo katika mabasi yao," anaeleza.

Anafafanua mfumo huo unavyofanya kazi, kwamba inarekodi spidi kuanzia dereva atakavyoendesha, lakini mwendokasi unapofika kasi ya kilomita 85 kwa saa, kengele hulia kumtahadharisha mwendeshaji.

"Mfumo huu unaruhusu ufuatiliaji wa basi wakati huo huo likiwa safarini, kwani ofisa wa LATRA, mmiliki au Jeshi la Polisi, wanaweza kukaa ofisini na kufuatilia kila basi mwenendo wake na kuchukua hatua kwa wakati," anasema.

Kahatano, anafafanua kuwa, mfumo haulizuii gari kuvuka spidi iliyowekwa, lakini unahifadhi rekodi za kasi barabarani, mahali na muda anaosimama njiani.

### WANAOTETEA ABIRIA

Hassan Mchanjama, Mwenyekiti wa Chama cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA), anaeleza kuunga mkono juhudi zinazofanywa na wadau wa usafiri kusaka usalama wa abiria.

"Kama wadau wa usafiri, tunaunga mkono juhudi za kuhakikisha abiria anasafiri na kufika salama kule aendako na pia apate huduma sahihi, hivyo suala la VTS na tiketi za kielektroniki ni vya muhimu," anasema Mchanjama.

Anafafanua: "Tunaamini kwamba kuna mafanikio kwenye mfumo huo, ingawa zipo changamoto mbalimbali hasa zinazotokana na baadhi ya wamiliki wa mabasi kutotumia au kutofuatilia madereva wao, ili wasichezee mfumo huo katika mabasi yao."

Kuhusu ukatishaji tiketi za mabasi kwa njia za kielektroniki, anakiri kukubaliana na mfumo huo mpya, jambo wanaoamini itawaondolea abiria usumbufu wa walio nao kila mara.

"Hatua hii ya kuwapo tiketi hizo itaondoa wapigadebe vituoni, pia itakomesha wajanja wachache ambao wamekuwa wakipandishia abiria nauli kwa kujali maslahi yao zaidi," anasema.

Mwenyekiti huyo anasema, chama chao kimekuwa kikitoa elimu kwa abiria kujua haki zao, kuanzia usalama katika safari na hata kuepuka kuibiwa mali au kuzindishiwa nauli wanapotaka kukata tiketi.

AFYA

# Kinachofanikisha wenyeji wa Kagera wasisukumwe kusaka chanjo watoto

## •Mratibu Chanjo: Elimu yao kama darasani
## •Kutishana, kuigana wenyewe kumesaidia

**Na Jaliwason Jasson, BUKOBA**

***WIKI mbili zilizopita, safu hii ilikuwa na simulizi ya mafanikio ya huduma za chanjo katika Manispaa ya Bukoba yalivyovutwa nyuma kwa miezi kadhaa mwaka jana na kikwazo corona, iliyokuwapo nchini. Nini mzizi wa mkoa kukwea kilele? Pata simulizi ya kina.***

WAZIRI aliyebeba dhamana katika Afya, Jinsia, Wazee na Watoto katika serikali ya awamu iliyopita, Ummy Mwalimu, katika hotuba yake ya makaridio ya mapato na matumizi mwaka 2018 /2019 bungeni, alianika namna ambavyo walipiga hatua katika huduma ya chanjo, kati ya Julai, 2018 hadi Machi, 2019.

Waziri alitamka, Mpango wa Taifa wa Chanjo unaohakikisha kuwapo vifaa vyote kwa kila mikoa na lengo ni kuhakikisha walengwa watoto wa umri chini ya mwaka mmoja wapatao 2,013,744 wanapata chanjo zote zinazotakiwa.

Alisema, takwimu zilizotolewa na mkoa au wilaya yoyote iliyoripoti kuishiwa chanjo au vifaa vyake, Wizara ya Afya ilichukua hatua na kuhakikisha huduma ya chanjo ya watoto chini ya mwaka mmoja, hata ikafanikiwa kwa asilimia 98 ya lengo lake.

Alisema, wizara iliendelea na ukarabati wa maghala ya kutunza vifaa chanjo yaliyopo Dar es Salaam, ikiwa sehemu ya kuanzisha uzalishaji chanjo nchini.

Katika hotuba hiyo, wizara ilitumia Sh. bilioni 13.9, kununua majokofu yanayotumia nishati ya jua 1,385 na kusambazwa katika halmashauri zenye uhitaji, pia vifaa vya kielektroniki (tablet) kutunza taarifa za chanjo katika ngazi ya zahanati na vituo vya afya nchini.

Waziri Ummy alitaja mikoa iliyonufaika na majokofu ni Dodoma, Geita, Kigoma, Lindi, Tanga, Mtwara, Mbeya, Shinyanga, Songwe, Singida, Mara, Mwanza, Pwani na Kagera.

**HALI ILIVYO KAGERA**

Takwimu za kitaifa za mwaka 2015 zilionyesha Mkoa wa Kagera ulitoa chanjo kwa watoto asilimia 87.5 huku kitaifa kundi hilo walikuwa asilimia 75.7.

Mratibu wa Huduma ya Mzazi na Mtoto wa Mkoa wa Kagera, Neema Kyamba, anataja siri ya mafanikio ya chanjo, ni wanavyofuata ratiba za chanjo na kuzingatia wakati.



Moja ya kliniki za watoto iliyopo mkoani Kagera.

Neema anataja mzizi mwingine wa mafanikio ni huduma za mikoba wanazotumia kwa kuwafuata walioko mbali na anawasifu kinamama wa mkoa kuwa waelewa wa chanjo, wanaozingatia upatikanaji wake.

Pia mtaalamu huyo ambaye anatoa elimu ya chanjo, anataja kingine kichachoukweza mkoa ni kuwafikisha vijijini watoa huduma.

Anasema, katika eneo hilo wanajitahidi kwa zaidi ya asilimia 90 wakizingatia watoto kupata chanjo pasipo kusukumwa na wataalamu, kazi kuu ikiishia kukumbushana chanjo.

Mratibu Neema anaeleza ushuhuda, wazazi wanaosaidia wenzao kwa kutoa elimu ya chanjo inayomwepusha mtoto na madhara ya magonjwa hatari, vivyo hivyo kila kituo kimejiwekea ratiba ya madarasa ya kinamama kufanikisha chanjo za watoto.

Neema anadokeza maeneo muhimu ya masomo, yanagusa stadi za usafi, chanjo, lishe na namna mama anamwachia mtoto muda, kabla ya ujauzito mwingine.

Anasema huwa wanafanya tathmini kila mwezi, wakishirikiana na watoa huduma kwa kukagua mafanikio ya mikakati ya iliyowasaidia na kupanua wingi wa ufuatiliaji. Unapotokea mkwamo, wanadadisi chanzo chake.

Mratibu anadokeza baadhi ya magumu yanayowakwamisha, ni usafiri katika nyendo zao, pale wanapokutana na jiolojia ya milima, mabonde, pia adha ya mvua na maeneo yasiyofikika kirahisi.

**WAZAZI WAFUNGUKA**

Mkazi wa Mtaa wa Nyakanyasi mjini Bukoba, Katushabe Rwekaza, anasema katika jamii ya wenyeji hao sasa kuna mwamko mithili ya mila, mama hata anapojifungulia kijijini, mtoto anawahishwa kwenye chanjo.

Anasema, ni wajibu unaochukuliwa na jamii inayomzunguka wakimpeleka mtoto kwenye kituo cha afya akapatiwe chanjo.

Katushabe anaendelea: "Tunaogopa sana kukaa na mtoto bila kupatiwa chanjo tunafikiri atapata magonjwa ndio maana tunamkimbiza mtoto zahanati."

Anaeleza zamani wazazi walipuuza kuwajibikia huduma ya chanjo iliyopo kwa watoto wao, lakini ushuhuda wa matukio ya vifo katika jamii yao na elimu inayotolewa na wahudumu wa afya, sasa imeleta mabadiliko ya kitabia sasa wanawahi zahanati kupata chanjo.

Diana Richard, mkazi wa Kibeta Bukoba, anaunga mkono uhalisia kwamba hivi sasa kuna mafanikio kwenye chanjo, kwa kuwa wataalamu wa afya wanawapatia elimu ya kutosha.

Anasema, licha ya chanjo za watoto zinafanywa kwa sindano zenye maumivu makali makali kwao, bado haijawa kigezo cha kuwakatisha tamaa, kwani wanatambua vyema thamani yake kiafya.

Mama huyo anataja faida mojawapo ya chanjo, ni kuimarisha afya ya mtoto asipate magonjwa, akisifu tabia kuwa wazazi wengi wa sasa wanarithishwa na watangulizi wao, kwa kujifunza kuwaona na safari za kliniki wakiwa na watoto wao.

Mkazi wa Katoma, Bantulaki Kalikawe, anatamka kwamba 'suala la chanjo katika jamii halina ubishi' akiwa na ufafanuzi linagusa afya ya mtoto na kumwandalia msingi imara kwa afya yake.

Kalikawe anatumia fursa hiyo kuishukru serikali kwa kutoa fursa za chanjo kwa watoto wao kwa wakati sahihi na anaikumbusha kwamba, isisahau pembezoni wanakoishi jamii za wafugaji wa Kagera, kwa huduma kuwafikia watoto wao.

Mkazi wa Kashai, John Magezi, anasisitiza suala la chanjo lina ulazima anaouita wa asili, hivyo wanajamii wana ulazima kupeleka watoto zahanati, vituo vya afya na hospitalini kwa ajili ya chanjo.

Kemilembe Rwegasira, mkazi wa Bugabo Bukoba, anataja mzizi wa mafanikio Kagera kufanya vizuri kwenye chanjo, ni kuwatumia watoa huduma wanaosaidiana na wataalamu afya wa zahanati, vituo vya afya na hospitalini.

Pia, anataja msukumo mwingine kutoka simulizi za mitaani kwamba "Watu huambizana kuwa ukienda nchi jirani ukakosa, kitambulisho Watanzania wengi hutambuliwa kwa ile chanjo begani," kutokana na alama yake.

**ASASI ZA KIRAIA**

Mratibu wa Shirika la Community Development Initiatives (KCDI), Christine Nyangoma, anasema katika uboreshaji chanjo kwa watoto, huwa wanahamasisha kinamama kufikisha watoto wao kliniki.

Anasema, huwa wanaenda kliniki kuwapima watoto wakishirikiana na wataalamu afya. Hapo wanahoji kuhusu afya za mtoto na anapogundulika kupungua au kuongezeka uzito, wanadidisi mabadiliko hayo kwa ajili ya kuyafanyia kazi katika utoaji elimu afya.

Ofisa huyo anasema, kuna kipindi asasi yao iliamua kujenga zahanati katika Kijiji cha Kikukwe, Kata ya Kanyigo, wilayani Misenyi, lengo ni kuwasogezea karibu huduma za afya.



Mtoto akipatiwa chanjo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

AFYA

## MGANGA MKUU WA SERIKALI:

# Sasa kazi, tuone vitendo vya kila mmoja akiwajibikia wagonjwa

- Hospitalini wamuige waziri kutoa simu
- 'Whatsap' nyenzo rasmi ya kufuatiliana



Aliyekuwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akimsikiliza Halima Said, alipotembelea Hospitani ya Rufani ya Mwanyamala, Dar es Salaam, kusikiliza kero za wagonjwa.

**Na Yasmine Protace**

UNAPOZUNGUMZIA sekta ya afya, maana kubwa inaangukia maisha ya watu. Hata tafsiri pana ya kinachofanywa na Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MAMM) nchini, unaotekelezwa kwa wastani wa miaka 12 sasa, unaangukia hapo.

Mtazamo wake ni walau kila kijiji wakazi wawe jirani na zahanati inayowahudumia na katika kata kunakuwapo eneo la rufani, kituo cha afya, wilaya inapata hospitali na mkoa hospitali ya rufani, hali kadhalika ngazi ya rufani za juu na juu yake Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Lengo kuu hapo ni kutatua au kupunguza kero kutoka mikononi mwa jamii, jambo ambalo Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, anayesema ni jambo ambalo serikali ipo tayari kuzipokea.

Anafafanua kuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ipo tayari kupokea kero na malalamiko ya wananchi, endapo wameshindwa ama kusikilizwa au kusaidiwa na viongozi wa ngazi za chini na vituo vya kutoa huduma za afya waliko.

Ni angalizo lililojaa ufafanuzi, ambalo Prof. Abel Makubi alilitoa baada ya kufanya kikao kwa njia ya mtandao na viongozi wakuu wa sekta ya afya, kilichowajumuisha waganga wakuu wa mikoa na wilaya.

Wengine walioshiriki kikao hicho ni Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Huduma za Afya za Mikoa (RHMT) na wilaya (CHMT) na wakurugenzi wa hospitali za kitaifa na jumla ya washiriki ni 220, ajenda kubwa ikiwa ni kupunguza kero.

Prof. Makubi anasema, wananchi wana matumaini na serikali yao, jambo ambalo ni haki yao kusikilizwa na kutatuliwa kero kupitia watendaji kwenye vituo vyote vya huduma za afya nchini.

**SOTE TUBEBE MZIGO**

Mganga Mkuu anaongeza kuwa kamati zote zinapaswa kufanya tathmini za kero zote kwa muda wa wiki nne, kuzitatua, kuwasilisha ripoti ziarani pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa (TAMISEMI).

"Tunaanzisha utaratibu ambao sisi viongozi wa sekta ya afya tunaenda kutafuta kero kutoka kwa wananchi na kuzitatua. Hili ni agizo na tumekubaliana wasambae kwenye ngazi zote," anabainisha.

"Kuanzia zahanati vituo vya afya na kwenye hospitali, tunatakiwa kuhakikisha wananchi wapate huduma bora licha ya kuwa tumeboresha huduma kwenye vituo vyetu," anafafanua.

Prof. Makubi anasema ni utaratibu unaorahisisha kutatua kero za wananchi na kuwaupunguzia kero ambazo hazipaswi kuifika ngazi za juu kiutendaji, kama vile ofisi ya waziri, hivyo watendaji husika wanapaswa kujitafakari namna ya kutatua shida za wananchi.

"Tumekubaliana kuimarisha suala la uongozi, uwajibikaji na usimamizi, kwani kila mmoja ameona kuna upungufu kwenye usimamizi wa huduma za afya nchini.

"Hivyo, tumekubaliana kila kiongozi kuanzia taifa hadi vijijini kusimamia sehemu zenye upungufu, kwani wananchi wanahitaji mazuri kutoka kwetu. Hatuwezi kuwaridhisha kwa kila kitu, lakini tupunguze matatizo yao," anasema.



Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Abel Makubi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Upande wa vitengo vya huduma kwa wateja, Mganga Mkuu huyo wa Serikali, anasema kunahitaji maboresho zaidi na umma unahitaji kuchakata kero zote na kuzifanyia kazi.

Ni utekelezaji anasema unafuatwa kilichofanyika kubandikwa kwenye mbao za matangazo ya vituo vyao na wanapaswa kuwa hai wakati wote, kwa kuwa mwananchi wanataka huduma za afya kwamba namna ya ufanisi wanaotarajia.

"Viongozi hao pia wanatakiwa kukagua ndani ya hospitali zao kwenye maeneo ya kutoa dawa na stoo, kuona kama dawa zipo na zinawatosheleza wananchi na kama kuna wizi tuweze kuchukua hatua.

"Waende kwenye wodi na 'OPD' (wagonjwa wa nje) kuwasalimu wagonjwa na kama wana kero waziseme, ili wazitatue, pia maabara kuweza kuona kama vipimo vinafanyika," anasema.

Mganga Mkuu anataja ubunifu mwingine unajumuisha kutumia makundi ya mitandao ya simu na 'Whatsap' wataopokea na kushughulikia kero kwenye kila wilaya au mkoa husika, ili kila mwananchi aweze kutoa kero zake.

"Tumeagiza kuwe na namba ambazo zitatangazwa kwa wananchi. Pia, wawashirikie wananchi kupitia mikutano na kutaja namba zao, ili wananchi wajue wanawasilisha vipi malalamiko yao," anasema.

Prof. Makubi ana ufafanuzi kwamba wananchi wanapaswa kujenga imani na kuwaamini watendaji wote wa sekta afya, hasa kwa kufuata nyayo za waziri mwenye dhamana aliyetangaza namba zake za kupokea malalamiko.

Kwa mujibu wa Mganga Mkuu, ndani ya wiki mbili, Waziri Dk. Dorothy Gwajima, aliyetangaza namba ya malalamiko mwishoni mwa mwaka jana, 0734124191 na ameshapokea jumla ya malalamiko 3,000 yanayohusiana na huduma za afya nchini, kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Ni katika kipindi hicho alichotoa namba, aliitisha kikao na viongozi wakuu katika wizara yake na eneo mojawapo alilowekea msisitizo ni matumizi sahihi ya bajeti ambazo wakuu wa vituo vya afya wamepewa kufanikisha majukumu yao ya kuhudumia umma.

Aidha, ni kipindi ambacho Mfamasia Mkuu wa Serikali, alihimiza Desemba 31 mwaka jana, wenye maduka ya dawa ambao hawajasajiliwa kuchukua hatua, ikiwa sehemu ya juhudi kusaka ufanisi wa huduma bora ya kazi ya kuhudumia mhitaji wa dawa, ambaye ni mgonjwa.

AFYA

## SHIDA IKO KWENYE SAHANI...

# Utamaduni na kanuni zisizofaa za ulaji, mvuto wa magonjwa yasiyoambukizwa

- Zaingia taratibu, zina ubishi kutoka
- Nyama iko maarufu mezani, lakini...

**Na Michael Eneza**

JITIHADA zimekuwa zikifanyika miaka mingi kuielimisha jamii kuhusu matumizi ya lishe bora ili kuzuia magonjwa yasiyoambukizwa.

Kuna siku kadhaa za kimataifa zimewekwa ili kuwezesha uwapo wa mitandao ya kuandaa mijadala na harakati za aina tofauti kuhusu umuhimu wa lishe bora, lakini kiwango cha ufaulu kimebaki suala la mjadala.

Taasisi za afya za kiserikali na vikundi huria bado vinaendelea kuhimiza lishe inayofaa, ingawa havina mamlaka kamili ya kisheria, katika ukiukwaji wake ambao huzaa matokeo magonjwa yasiyoambukizwa yanakuwa na gharama kubwa.



Aina tofauti za mlo ambazo watu wanatumia, kwa kiasi kikubwa huegemea kwenye ladha.
**PICHA ZOTE: MTANDAO**

### MTIHANI WA UDHIBITI

Wataalamu wamekuwa wakitafuta chanzo cha kushindwa kufuata maelekezo ya lishe bora kwa ajili ya afya ya muda mrefu, kwani magonjwa yasiyoambukizwa hujijenga taratibu mwilini, yakichukua muda mrefu.

Athari yake, inachukua sura pale yakishajikita mwilini katika mfumo wa mzunguko wa damu, inakuwa ngumu kuondolewa, kwani sababu yanakuwa sehemu ya kilichoko mwili.

Tabu iliyoko katika mfumo wa maisha ni kwamba, kinachofanyika katika mwili wa binadamu kinaanza na mazoea, kana kwamba ndicho kinachotakiwa, wakati ukweli ulioko kwamba ni uharibifu tu.

Sehemu ya tatizo kubwa zaidi kwa mwanadamu, ni namna ya kupanga viwango vya sukari na mafuta, kulinganisha na mahitaji halisi mwilini.

Kutumia lishe ya aina fulani kwa wingi au kila wakati kunauzoesha mwili kuikubali aina hiyo ya lishe na kuondoa vipingamizi vinavyohusu ama sukari au mafuta kwa viwango vinavyotakiwa mwilini.

Ni kuanza ratiba au mpangilio mpya wa kuchukua chembe za lishe hizo kutokana na upatikanaji wake, hali inayofanya sukari au mafuta kutawala mwilini, kuzuia mtiririko wa kawaida wa sukari au mafuta kuingia, kutumika na kutolewa mwilini.

Kisha inaelezwa, kiwango kingine kinaingia na kufuata mkondo huo huo na inapofikia mahali mwili unakosa uwezo wa kudhibiti sukari au mafuta, zenyewe ndizo zinautawala mwili. Ndio hatua ya magonjwa kuanza kuchukua nafasi yake.

### WIGO WA UTAFITI

Katika nchi zinazoendelea kama barani Afrika, hakuna utafiti unaofanyika kuhusu lishe, mazoezi na afya, kulinganiasha na kulikopiga hatua zaidi ya maendeleo kama bara Ulaya na ufuatiliaji wa kina unafanyika kutoka taasisi tofauti za tiba za serikali na binafsi.

Matokeo yake hutumika kama vigezo vya kupitisha au kupinga hitaji la mabadiliko ya sheria kuhusu bidhaa za vyakula na vinywaji, ambako kuna makundi tofauti, mathalani penye mlo, bidhaa za nafaka na nyama upande mmoja, pia vinywaji baridi na vilevi upande mwingine.

Nguvu ya sheria ipio katika maeneo kama kila badiliko la kodi, huwezesha aina moja ya bidhaa na kuvuruga matazamio ya bidhaa ya aina nyingine. Hivyo, kuna vita ya kibiashara inayojificha katika tafiti za lishe.





Kwa mfano kuna tafiti zinazotajwa na hata kaulimbiu ya taasisi tofauti za afya kuwa 'sukari ni sumu' ikidaiwa iwekewe sheria inayohusu ununuzi na matumizi yake, lakini kuna sura ya pili majibu, kwamba siyo rahisi mwanasiasa au mwanaharakati anayetaka mabadiliko kuashiria kudhihirisha ukweli ulioko.

Inajenga tafakari ya hoja kati ya sukari na mbadala wa asali na siagi mwilini na matokeo yake. Katika nchi nyingi zilizoendelea kama Ulaya, nyama hasa nyekundu ni chakula halisi na msingi wa lishe ya kila siku, mfano mmojawapo ni mlo mkuu ama mchana au usiku huwa ni nyama, ikiandamana na mboga za kuusindikiza.

Watumiaji lishe ya nafaka kama ugali au wali kuwa msingi na inachosindikiza ni nyama, samaki ua maharagwe walio nayo ni wahamiaji.

Kutokana na kupenda kutumia nyama kama chakula kikuu takriban kila siku, kinatajwa kuchochea magonjwa ya moyo, watu wengi wanajaribu kutumia lishe za ziada kupunguza athari hizo.

### WANAKOKWAMA WALAJI

Pia vitamini vinaandaliwa maabara, badala ya kupatikana kutokana na lishe halisi na baadhi ya wataalamu wanatia shaka uwezo wake kumsaidia mhusika.

Msisitizo wa kitaalamu ni kwamba mabadiliko ya lishe na mazoezi ni muhimu, ila bado kuna tatizo la watu kufahamu hasa ni nini kinachozuia watu kuchukua mwekeleo wa 'lishe bora' na siyo 'bora lishe

Kwanini watu wanazama katika nyama? Kuna sababu muhimu mbili zinazoshindana. Moja ni utamaduni kwa maana ya mapokeo lishe na mazoea katika maisha ya mtu binafsi, hali ambayo pia inajichanganya na hisia za kitabaka, kula ni kielelezo cha umaskini na aliyeko vizuri kiuchumi anakula nyama.

Hisia hizo zinapotawala mtu kukubali cha upande wa pili kisayansi, chakula kuleta shida katika msukumo wa damu, kisukari.

Lakini kuna wanaorekebisha fikra na kujielimisha kwenda katika ukweli kufahamu kwamba tahadhari ya lishe ni muhimu zaidi, ingawa kuchukua hatua kudhibiti bado ni shida. Mathalan, mtu mzima anaona aibu kufanya mazoezi kukimbia hadharani, wengine wanabaki kuugua kimyakimya.

Katika nchi zilizoendelea, kuna uwezekano mkubwa zaidi wa elimu kuleta mabadiliko katika mazoea lishe. Miongoni mwa makundi makubwa ya watu na utafiti zinaonyesha kuwa waliosoma zaidi, wako makini kwa mausala hayo kuliko wenye elimu ya kawaida, iwe sekondari au ufundi).

Hata hivyo, kuna tatizo sugu la lishe kwa sababu wengi wanajiwekea mipaka kwa kuhofia magonjwa na siyo kwa kupenda lishe mbadala, hivyo wanakuwa kama mtu anayetaka kuacha sigara halafu aporomoke tena, aendelee, aache tena.

Ni hapo anachukua hatua ya vigezo vingine kama vile vya kitabaka au kijinsia kuhoji mfano wa wanaoshiriki urembo au hata warembo kwa jumla, wana uwezo kiasi gani wa kujizuia lishe kwa mazoea hata wakapunguza unene na uzito?



# DUWASA kuongeza visima vya maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA), imejipanga kuwapo na huduma ya maji ya uhakika kwa kuongeza visima ili kukabiliana na ongezeko kubwa la mahitaji ya maji.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu mikakati ya uboreshaji huduma ya maji jijini humo, Mkuu wa Kitendo cha Mawasiliano wa Mamlaka hiyo, Sebastian Warioba, alisema hadi sasa kuna visima 10 ambavyo vimeanza kuchimbwa eneo la Zuzu na Ihumwa.

"Tumefanikiwa sana tumepata visima vina maji ili kuhudumia eneo lile la Zuzu na kwa eneo la Ntyuka tunataka kufanya hivyo hivyo, lakini kwa upande wa Ihumwa tunataka tukichimba tunaweka na pampu na mabomba ili maji yaende kwenye tangi ambalo liko Njedengwa Mji wa uwekezaji," alisema.

Alisema kuna visima vingine 10 vitachimbwa kwenye maeneo mbalimbali katikati ya mji ili kuongeza kiasi cha maji kwenye mitandao.

"Pia tumeshirikiana na wenzetu wa mabonde wa Wizara ya Maji tumeainisha kuna visima vya miaka ya nyuma kama vile pale Nzuguni, mpaka sasa tumeshaainisha visima 13 ambavyo kulikuwa na shida ya maji Dodoma," alisema.

"Baada ya kupata maji ya kutosha visima vile vilikuwa havitumiki kwa hiyo tunachokifanya sasa tumevitambua, tumeanza na kile cha Nzuguni na vingine tumeweka wataalamu ambao wanavisafisha kwa maana ya kukarabati na kupima kiasi cha maji yanayotoka na ubora wake halafu baadaye tunafunga pampu kwenye visima," alisema.

Alitoa wito kwa wanaotumia maji kinyume na sheria kuacha mara moja kwa kuwa watakapobainika watachukuliwa hatua za kisheria.



Kinamama wachuuzi wakifanya biashara katika mazingira hatarishi kiafya kutokana na kuzungukwa na matope katika soko la Sabasaba, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wakazi Nzuguni waomba ujenzi daraja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kujenga daraja jingine katika Kata ya Nzuguni, jijini Dodoma ili kukamilisha vivuko vya mitaa inayopitiwa na korongo linalosababisha wananchi kushindwa kuvuka hasa kipindi cha mvua.

Wananchi hao ikiwamo wanafunzi hulazimika kukaa kwa muda mrefu pembezoni mwa korongo hilo, ili kusubiri maji yapungue, wavuke kuelekea upande wa pili wenye huduma.

Wakizungumza na Nipashe jana, wananchi hao walisema mitaa ya kata hiyo inazungukwa na korongo kubwa ambalo wakati wa mvua hujaa maji na kusababisha wananchi kuhofia kuvuka kwenda upande wa pili.

Mmoja wa wananchi hao, Jasmine Shamwepu, alisema pamoja na serikali kujenga daraja moja linalounganisha mitaa ya Nzuguni B na C, inahitajika lingine linalounganisha Nzuguni A na B ili kukamilisha vivuko kwenye kata hiyo.

"Hili korongo hapa ambapo upande wa pili kuna Shule ya Msingi Nzuguni kipindi hiki cha mvua hakuna anayevuka, watu wenye magari wenyewe wanasubiri hadi maji yapungue ndio wavuke, tunaomba serikali itusaidie kupata daraja jingine la pili ambalo litasaidia kuunganisha mitaa ya Nzuguni A na B," alisema. Alisema kuna watu waliwahi kupoteza maisha kwa kusombwa na maji katika eneo hilo.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alikagua ujenzi wa daraja la Nzuguni ambao umesaidia kutatua adha ya muda mrefu iliyokuwa ikiwakabili wananchi hao.

Aliahidi kuendelea kutatua kero ya miundombinu katika eneo hilo ili kuondoa adha kwa wananchi wakati wa mvua.

"Tuliahidi wakati wa kampeni kwamba tutasimamia ujenzi wa daraja hili na leo ndani ya miezi miwili tangu mlipotupa ridhaa kazi hii inaelekea kukamilika," alisema. Aliishukuru serikali kupitia Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) kwa usimamizi wa mradi huo ambao umekuwa mkombozi kwa wananchi hao.

Akitoa maelezo ya awali, diwani wa kata hiyo, Alloyce Luhega, alisema pamoja na ujenzi huo pia kuna ukarabati wa barabara za ndani za kata hiyo ambazo zitagharimu Sh. milioni 700.

# Chamwino yajipanga kutengeneza barabara zote

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chamwino, imejipanga kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara zote korofi zilizoharibiwa na mvua inayoendelea kunyesha.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Yarerd Swert, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya wakazi wa Kijiji cha Loje na Igunguli wilayani humo kwa kukosa mawasiliano kutokana na barabara hiyo kuwa mbovu na madaraja yake kukatika.

Alikiri kuwa hali ya miundombinu ya barabara na madaraja kwenye wilaya hiyo siyo rafiki kwa watumiaji wa vyombo vya moto na watembea kwa miguu kutokana na kuharibiwa na mvua.

Alisema kuwa halmashauri hiyo itahakikisha inafanya matengenezo ya barabara hizo ili zipitike wakati wote.

"Ni kweli kuna barabara ambazo ndani ya halmashauri hii ya Chamwino ni mbovu kwa hivi sasa hii ni pamoja na baadhi ya madaraja kutopitika baada ya kuharibiwa na mvua zinazoendelea kunyesha kwa hivi sasa," alisema.

"Halmashauri imejipanga kupitisha bajeti ya kutengeneza barabara zote korofi pamoja na madaraja ila hajui Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) wamefikia hatua gani kwa upande wao kwa ajili ya mategenezo yake."

Awali, Wakazi wa Kijiji cha Loje na Igunguli wilayani humo, walisema hivi sasa hawana mawasiliano kati ya Loje na Igunguli kutokana na ubovu wa barabara na madaraja yaliyopo kukatika.

Mathayo Mazengo, mkazi wa kijiji cha Loje alisema kutokana na ubovu wa barabara hiyo shughuli zao zimesimama ikiwamo za kilimo na uvuvi ambao wengi wao hujishughulisha na shughuli hizo.

"Kijiji cha Igunguli kuna bwawa linalotumiwa kwa shughuli za uvuvi, hivi sasa hakuna kazi yoyote inayofanyika kutokana na kutopitika kwa barabara hiyo hali ambayo imewafanya vijana kukosa kazi na hata kwa upande wa halmashauri yenyewe inakosa kukusanya mapato," alisema.

Naye Diwani wa Viti Maalum wilayani humo, Hild Kadunda, alisema kutokana na ubovu huo, kata hiyo inakosa makusanyo yaliyokuwa yakipatikana kutokana na shughuli za uvuvi unaofanyika kwenye bwawa la Igunguli.

"Tunategemea halmashauri kwa kushirikiana na TARURA wataitengeneza barabara hii ambayo ni muhimu kutokana na shughuli zinazofanyika za uvuvi ambao umekuwa ukiiletea halmashauri mapato kwa ajili ya maendeleo yake," alisema.





## 'Kila mamlaka ya maji ipande miti milioni 6'

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

NAIBU Waziri wa Maji, amezitaka mamlaka za maji nchini kupanda miti isiyopungua milioni sita kwenye vyanzo vya maji, ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira unaochangia vyanzo vya maji kukauka.

Maryprisca Mahundi alitoa agizo hilo juzi mkoani Mbeya wakati wa upandaji wa miti kwenye vyanzo vya maji ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Mbeya.

Mahundi alisema mikoa yote inatakiwa kupanda miti kwa lengo la kulinda vyanzo vya maji na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanachangia vyanzo kukauka.

"Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Mbeya imeanzisha utaratibu mzuri wa upandaji miti kwenye vyanzo mbalimbali vya maji, utaratibu huu unapaswa kutekelezwa kwa mikoa yote nchini," aliagiza.

Aliwaomba wananchi na watumishi wa mamlaka hiyo kutunza miti iliyopandwa kwenye chanzo cha maji cha Nzovwe kilichoko Kata ya Mwakibete na kuagiza mamlaka kusogeza huduma ya maji maeneo hayo kuliko ilivyo sasa ambapo hakuna huduma hiyo licha ya kuwa karibu na chanzo.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Mbeya, Ndele Mengo, alisema miundombinu ya maji imesambazwa kwa asilimia 90, lakini wananchi wanaopata maji ni asilimia 57, hivyo tatizo la upatikanaji wa maji bado ni kubwa.

Aliiomba serikali kuendelea kuisaidia mamlaka hiyo kuboresha miundombinu ya maji ili ianze kufanya kazi katika baadhi ya maeneo ambayo hayapati huduma hiyo hadi sasa.

Chifu wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Rocket Mwashinga, aliiomba serikali kuwashirikisha machifu kwenye ulinzi wa misitu hiyo pamoja na vyanzo vya maji ili kuepuka athari zinazochangiwa na shughuli za kibinadamu.

Awali, kulifanya msako na kumkamata mtu mmoja aliyejiunganishia maji kinyume cha sheria ikiwa ni mwendelezo wa kukamata watuhumiwa wa aina hiyo.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akisalimiana na baadhi ya wakulima na wafugaji wanaofanya shughuli zao kwenye Ranchi ya Usangu iliyopo Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Waziri aagiza wakulima wapewe ranchi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Profesa Elisante Ole Gabriel, kuandaa utaratibu mzuri wa kukodisha mashamba ya malisho (banchi) kwa wakulima ambayo wako tayari kulipa kodi ya mashamba hayo kwa serikali.

Ndaki alitoa agizo hilo jana alipohitimisha ziara yake ya siku mbili mkoani Mbeya, akitembelea eneo la ranchi ya Usangu iliyoko wilayani Mbarali na kuzungumza na wakulima na wafugaji kujua vikwazo vinavyowakabili.

Wakulima wa Bonde la Usangu walimweleza Waziri Ndaki kuwa kwa sasa wanakodisha mashamba ya ranchi kutoka kwa wawekezaji na kwamba gharama ni kubwa, hivyo waliiomba serikali kuwamegea eneo lao kwa ajili ya kilimo.

Mmoja wa wakulima hao, Pascalina Mhagama, alisema ekari moja ya shamba wanakodishiwa Sh. 50,000 na kwamba baada ya mavuno, hutakiwa kutoa kiasi cha mpunga wanaovuna kwa wawekezaji hao.

Alisema hali hiyo inawaumiza, hivyo wanaiomba serikali kwa kushirikiana na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), kumega baadhi ya maeneo ya ranchi ili yatumike kwa ajili ya kilimo.

Kutokana na malalamiko hayo, Waziri Ndaki alielekeza kuwa maeneo yote yaliyoshindwa kuendelezwa kwa ajili ya malisho ya mifugo, yakodishwe kwa wakulima ili kuleta mapato kwa serikali.

Alisema kwa sasa wawekezaji wengi wana malimbikizo ya madeni na hivyo wanyang'anywe maeneo hayo na wakodishiwe wakulima ambao watakuwa wanalipa fedha kwa serikali.

"Ranchi ya Usangu ina jumla ya vitalu 16, lakini ukifuatilia vitalu hivi havifanyi kazi kwa mujibu wa mkataba, ni maalum kwa ajili ya malisho ya mifugo badala yake wameamua kuwakodishia wakulima na wanachukua fedha ambazo serikali hainufaiki nazo.

"Licha ya kuchukua fedha kutoka kwa wakulima, bado wana madeni. Sasa ninaagiza vitalu vyote vilivyoshindwa kutimiza masharti ya mkataba, vikodishwe kwa wakulima ili serikali iendelee kupata fedha," aliagiza.

Akipokea maelekezo hayo, Katibu Mkuu Profesa Ole Gabriel alisema atafanya mazungumzo na Katibu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuangalia namna bora ya kugawa maeneo hayo ya ranchi nchini, yaanze kutumika kwa ajili ya kilimo.

Alisema suala hilo litashughulikiwa na kuwatoa hofu wakulima walioomba kuwa watapewa na kuwahakikishia kuwa wawekezaji walioshindwa kulipa madeni ya NARCO, lazima wataondolewa.

Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Francis Mtega, alisema ardhi ya Mbarali ni ndogo kulinganisha na mahitaji ya wakulima, wafugaji na wawekezaji.

Aliiomba serikali kuandaa utaratibu mzuri wa kugawa maeneo hayo ili kila kundi linufaike na ardhi hiyo na kuepusha migogoro ya mara kwa mara baina ya wafugaji na wakulima.

Aliwataka wawekezaji kuwa waaminifu na kulipa madeni yote wanayodaiwa na serikali na kwamba kwa kufanya hivyo, kutaongeza mapato na huduma za jamii zitaendelea kuboreshwa.

# 61 mbaroni wakituhumiwa wahamiaji haramu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limewanasa watu 61 wanaodhaniwa ni wahamiaji haramu kutoka Ethiopia, wakiwa wanasafirishwa kwenda nchi jirani ya Malawi kwa kutumia lori la mizigo, huku dereva wa gari hilo pia akishikiliwa kwa kosa la kuwasafirisha.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika Kituo Kikuu cha Polisi cha Mkoa wa Mbeya, Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Jerome Ngowi, alisema watuhumiwa hao walikamatwa juzi katika kizuizi cha magari kilichoko Kijiji cha Gari Jembe Barabara Kuu ya Tanzania-Malawi.

Alisema watuhumiwa hao walikuwa wamefichwa kwenye lori aina ya Scania lenye namba za usajili T. 509 AZZ ambalo lilikuwa linaendeshwa na dereva ajulikanaye kwa jina la Rabdi Ramadhani (48), mkazi wa Unga Limited mkoani Arusha.

Alisema polisi waliokuwapo kwenye kizuizi hicho, walimsimamisha dereva huyo ili wakaguwe gari hilo na walipomhoji kuhusu mizigo aliyobeba, alisema amebeba bidhaa mbalimbali za dukani.

Kamanda Ngowi alisema polisi walimlazimisha dereva kufungua mlango wa nyuma wa gari hilo na ndipo wakabaini kuwa alikuwa amewabeba wahamiaji hao.

Alisema mbinu ambayo dereva huyo aliitumia ni kupanga maboksi kadhaa ya bidhaa za dukani mlangoni pamoja na mapipa na kisha akawaficha wahamiaji hao ndani ili wasionekane.

"Dereva huyu baada ya kubaini kuwa amegundulika, alianza kuwashawishi askari wetu wapokee rushwa ya Sh. milioni tatu lakini kwa sababu ya maadili yao walikataa, alipanda mpaka Sh. milioni 30 bado walikataa na wakamkamata," alisema Kamanda Ngowi.

Alisema baada ya kumhoji dereva wa gari hilo, alieleza kuwa alikuwa anawapeleka katika Mji wa Kasumulu wilayani Kyela uliopo mpaka wa Tanzania na Malawi.

Alisema jeshi hilo linaendelea kufanya mahojiano na dereva huyo ili kubaini mtandao mzima wa biashara haramu ya kusafirisha binadamu.

Kamanda Ngowi alisema wahamiaji hao walikutwa wakiwa na hali mbaya kiafya kutokana na kusafiri umbali mrefu bila kula chakula pamoja na kuhifadhiwa kwenye gari ambalo halina dirisha wala mlango uliokuwa wazi kwa ajili ya kuruhusu hewa kuingia.

Aliwataka madereva kuacha kuwasafirisha wahamiaji haramu, huku akiwataka wamiliki wa magari kutoruhusu magari yao kutumika kwa shughuli hiyo kwa maelezo kuwa ni kinyume cha sheria na adhabu yake ni kulipa faini, kwenda jela na magari yanayotumika kutaifishwa.

Oktoba 22 mwaka jana, watu 22 walikamatwa wilayani Mbarali na wengine 57 walikamatwa Desemba 15, mwaka jana, wilayani Rungwe, wakidaiwa ni wahamiaji haramu kutoka Ethiopia.





# SMZ kufufua uchumi hatua kwa hatua

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuchukua juhudi kubwa za kufufua uchumi hatua kwa hatua kwa kupitia sekta zake mbalimbali.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, alisema hayo juzi katika hotuba yake ya maadhimisho ya miaka 57 ya Mapinduzi wakati akiwahutubia wananchi kupitia vyombo vya habari.

Alisema hivi sasa, Zanzibar inaendelea kushuhudia ongezeko la makusanyo ya kodi kuongezeka kutoka Sh. bilioni 22 mwezi Oktoba hadi kufikia Sh. bilioni 36.9 Desemba, 2020 yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRB).

Dk. Mwinyi alisema sekta ya utalii imeendelea kuimarika, na iliweka lengo la kupokea watalii 250,855 ifikapo Desemba 2020, baada ya kuzingatia mwenendo wa maradhi ya Covid-19 ndani na nje ya nchi na hadi Novemba 2020 jumla ya watalii 212,050, wametembelea Zanzibar sawa na asilimia 85 ya makadirio.

Alisema pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta hiyo bado ipo fursa ya kuindeleza na serikali itasimamia kwa karibu uratibu, utangazaji na uendelezaji wa sekta hiyo ili itoe mchango mkubwa zaidi kwa Wazanzibari na uchumi kwa ujumla.

Alisema serikali inalitafutia ufumbuzi tatizo lililojitokeza la kuchelewa kupatiwa wageni huduma za msingi wanapofika katika uwanja wa ndege na kuwasababishia usumbufu, suala la kuwapo kwa huduma za zimamoto za uhakika kiwanjani hapo litashughulikiwa na kero nyingine zinazowakuta watalii wanapoingia nchini kwa kuzipatia ufumbuzi.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha wageni wanafurahia makazi yao Zanzibar jambo ambalo litachochea kupata watalii wengi wanaokaa kwa muda mrefu na kupendelea kurudi wanapohitaji kufanya hivyo.

Alisema vilevile serikali, itahakikisha sekta ya utalii inakuwa kichocheo kikubwa cha ukuaji wa sekta ya uchumi wa buluu.

Akizungumzia suala la biashara, Dk. Mwinyi alisema, jumla ya bidhaa zenye thamani ya Sh. 62,221,261,713, zilisafirishwa kwenda nje ya nchi, Januari hadi Novemba mwaka 2020, ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya Sh. 33,277,617,078, mwaka 2019 kwa kipindi kama hicho.

Alisema mchango wa sekta ya viwanda katika jumla ya Pato la Taifa umeongezeka kufikia asilimia 18.9 mwaka 2019 na serikali itaendelea na juhudi za kushawishi wawekezaji wa ndani na nje, kuja kuwekeza katika sekta ya viwanda.

Pia serikali kupitia Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), imeendelea kuchukua hatua za kudhibiti ubora wa bidhaa zinazotengenezwa au kuingizwa Zanzibar kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

Alisema, katika kipindi cha miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar, inajivunia kuimarika kwa huduma za elimu kwa kuongezeka shule za msingi na za sekondari kwa kiwango kikubwa na pia kuanzisha vyuo vikuu.

Dk. Mwinyi alisema pamoja na jitihada za serikali inazochukua katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii kama vile umeme na majisafi na salama, bado mahitaji ya huduma hizo kwa wananchi ni makubwa. Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itahakikisha sehemu zote ambazo hivi sasa zinakosa huduma za umeme na maji zinapata kwa mujibu wa mahitaji ya wananchi.



Mkulima Kassim Abdalla Ali akichangia mada wakati wa mkutano wa kuutambulisha mradi wa viungo, mboga na matunda unaotekelezwa na Taasisi za People's Development Forum, Community Forests Pemba na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, kwa ufadhili wa umoja wa Ulaya na kusimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa wakulima wa shehia ya Kiungoni, wilayani Wete, mkoa wa Kaskazini Pemba jana. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# Wakulima wafurahia mradi wa viungo

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

WAKULIMA wa Shehia za Kiungoni, Kinyikani, Pandani na Pembeni, Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba, wamesema mradi wa viungo, mboga na matunda katika shehia zao utasaidia kurejesha hamasa ya uzalishaji wa bidhaa za kilimo hicho tofauti na sasa wanapokabiliwa na matatizo ya ukosefu wa masoko pamoja na miundombinu duni ya uzalishaji.

Waliyasema hayo jana kwa nyakati tofauti wakati wa mkutano ya kuutambulisha mradi huo kwa wakulima wa shehia hizo na kwamba mradi huo umekuja katika muda mwafaka wakati wakulima wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa soko la kuuzia bidhaa wanazozizalisha shambani jambo ambalo husababisha kupata hasara zaidi kuliko faida.

Ali Said Khamis, kutoka Shehia ya Kiungoni alisema ujio wa mradi huo utasaidia kubadilisha maisha yao ikiwa ni pamoja na kuongeza hamasa kwa wakulima kuendelea uzalishaji, kwa kuwa wengi wanashindwa kuendelea na shughuli hizo kutokana na ukosefu wa soko la uhakika pamoja na miundombinu mibovu ya kuwezeha kilimo cha kisasa.

"Kwa kweli sisi wakulima tunashukuru sana na tunaupokea mradi huu kwa mikono miwili kwani tunaamini unakuja kutatua kilio chetu cha siku nyingi ambacho ni soko. Tunazalisha sana mazao, lakini hatuna sehemu ya kuyauza na kusababisha kuozea majumbani mwetu," alisema.

Alisema kuwa kwa muda mrefu wakulima wengi Zanzibar wameshindwa kuendelea kiuchumi kutokana na kulima kilimo kisicho na tija na kusababisha wengi wao kukata tamaa na uendelezaji wa shughuli hizo.

"Tegemeo letu wengi ukiachilia mbali kazi za Pwani shughuli nyingine tunayoitegemea sisi wanyonge ni kilimo, lakini kilimo hiki kwa muda mrefu kimeshindwa kutusaidia kutatua matatizo yetu kwenye familia kutokana na kutokuwapo kwa miundombinu mizuri ya kuwezesha kilimo chenye manufaa," aliongeza.

"Nimelima shamba langu la matikiti na nyanya mpaka sasa yamekomaa na nimeyavuna, lakini nimerundika ndani yanaoza tu sina sehemu ya kuuza, bidhaa tunazo, lakini pa kuuza hatuna. Hivyo tunaomba sana mradi huu uje utusaidie kutatua changamoto hizi tunaumia sana wakulima."

Naye Mtumwa Busra Moh'd, alisema wanawake watakuwa mstari wa mbele kuchangamkia fursa hiyo kutokana na mradi huo kuwalenga wanawake zaidi na kuwasaidia kukuza vipato vyao.

Mapema akitambulisha mradi kwa wakulima hao, Ofisa Kilimo wa Mradi, Yahya Khatib Suleiman, alisema umekuja kwa lengo la kutatua matatizo yanayowakabili wakulima kwa muda mrefu ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa masoko, uzalishaji kwa wingi wa bidhaa na zenye ubora unaotakiwa kukidhi mahitaji ya soko.

Naye Ofisa Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika mradi huo, Asha Mussa Omar, alisema mradi huo umeweka kipaumbele zaidi kwa wanawake na vijana kutokana na matatizo yanayowakabili katika sekta ya kilimo.

"Mradi huu unalenga kuwafikia asilimia 55 ya wanawake kati ya wote watakaonufaika na mradi huu kwa lengo la kuwaongezea wanawake fursa za kimaendeleo," alisema.

## KMKM yakamata 3 wakisafirisha mafuta ya kula

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KIKOSI Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) kimewakamata watu watatu wakiwa na madumu 180 ya mafuta ya kula wakisafirisha kwa njia ya magendo, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja.

Akieleza tukio hilo jana, Mkuu wa operesheni Kamandi ya Kusini KMKM, Luteni Mahmoud Muhsin Mahmoud, alisema askari wake waliokuwa katika doria za kawaida kikazi waliwakamata chombo hicho katika maeneo ya bahari ya visiwa Tele baada ya kukitilia mashaka.

Alisema chombo hicho kilikuwa kinaongozwa na nahodha Yussuf Akida (41), mkazi wa Bagamoyo, Adam Salum Mwembamba (29), mkazi wa Mkwajuni na Salum Moh'd Mtunguru, mkazi wa Mbagala Dar es Salaam.

Kamanda Muhsin aliwataka wananchi kuacha tabia ya kuvusha vitu au bidhaa kwa njia ya magendo kwa kuwa ni kosa kisheria na linaisababishia serikali kupoteza mapato yake.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kati Unguja, Marina Joel Thomas, alikipongeza Kikosi cha KMKM kwa juhudi inazo chukua kukabiliana na wahujumu wa uchumi kwa njia za magendo baharini na nchi kavu.

Alikitaka kikosi hicho kuendelea na kazi yao hiyo ili kuzuia mapato ya nchi yasipotee kwa wafanyabiashara ambao sio waaminifu na wanaokwepa kulipa kodi kwa kupitisha bidhaa zao kwa njia ya magendo.

Mkuu huyo alitoa onyo kali kwa wamiliki wa vyombo vya baharini na mabaharia ambao wanajihusiha na uvushaji wa biashara za magendo kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itatoa adhabu kwa kufuata sheria za magendo ikiwamo Sheria namba 1 ya mwaka 2003 ya KMKM ambayo imeweka wazi adhabu zinazostahiki kwa wanaojihusisha na kuvusha magendo.

Alisema sheria hiyo inatoa adhabu ya kutaifisha chombo na bidhaa iliyokuwa ikivushwa kwa njia ya magendo, kulipa faini sawa na bidhaa au mali iliyokamatwa na mtendaji wa kosa hilo kufungwa jela miaka saba na isizidi 25.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kushirikiana na serikali ya wilaya pamoja na kikosi cha KMKM mara wanapopata taarifa za uvushwaji wa magendo katika maeneo yao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

## ANATAFUTWA DEREVA

Anatafutwa dereva wa kike mwenye uzoefu wa kuendesha Magari Mjini Dar es Salaam. Mwenye nia na kazi hiyo apige namba 0784691605/0715691605.

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA KIJITONYAMA VYUMBA VIWILI INAJITEGEMEA, PLOT NA 712/1,BLOCK 46

MAWASILIANO 0787233272
0674927560

## TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSTITUTE

INATANGAZA MUHULA MPYA WA MASOMO KOZI,KILIMO,MIFUGO NA MAENDELEO YA JAMII.CHUO KIMESAJILIWA NA NACTE REG.PWF/041/ KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI. 0752761280/0767574701 AU WWW.TRACDI.AC.TZ

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHRISTIAN HENSCHEL** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **SUZUKI ESCUDO** yenye namba za usajili **T 365 DFP** chasisi namba **TX92W171039** engine namba **H27A12473**, yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**Polisi taarifa KAH/TR/RB/08/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GERALD MASHAKA EZEKIEL** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 916CSK** AINA YA WANHOO . KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
**TAARIFA YA POLISI GEI /MBO/TR/RB/1513/2021**

## CHAMPION AUCTION MART
## NOTISI/MNADA

KWA NIABA YA UNITY 3E SOLUTION (T) LTD MWANZA, TUNATOA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI KWA WADAIWA WALIOTAJWA HAPA CHINI WALIPE MADENI YAO WANAYODAIWA KWA MUDA MREFU.
ENDAPO WATASHINDWA KULIPA KWA MUDA ULIOTOLEWA, DHAMANA ZAO ZITAUZWA KWA MNADA WA HADHARA KWA RATIBA IFUATAYO:-

| NA. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | DICKSON NESTORY MJUNI | GARI TOYOTA IST T 214 CSX | 27/01/2021 SAA 5 ASUBUHI MKOLANI |
| 2. | RAMADHAN ABDALLAH NDEGERA | TOYOTA GAIA T 962 DCD | 27/01/2021 SAA 5 ASUBUHI MKOLANI |
| 3. | JAMES MBOGO MUMANGI | TOYOTA LAND CRUISA VX V8 T 996 DQD | 27/01/2021 SAA 5 ASUBUHI MKOLANI |

**MASHARTI YA MNADA:**
A. UKAGUZI UNARUHUSIWA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.
B. MALIPO NI 25% YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA SALIO LITALIPWA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14) TU.
C. ENDAPO MNUNUZI ATASHINDWA KULIPA SALIO KWA MUDA ULIOTOLEWA, ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI ZAKE NA NYUMBA ITAUZWA TENA.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA SIMU NA.**
**0755 902 273 / 0753 959 568 / 0755 244 442**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la
Nipashe kila siku

**OFISI ZA MATANGAZO**
Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com




OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HABARI KIMATAIFA

# UCHAGUZI MKUU UGANDA LEO: Mitandao kijamii yafungwa, Bobi Wine adaiwa kupanga kujiteka baada uchaguzi

**Kampala, UGANDA**

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni ameituhumu kampuni ya Facebook, kuchukua hatua ya kufunga akaunti kadhaa za viongozi na wafuasi wa chama tawala NRM.

Museveni alithibitisha kuwa aliagiza kampuni zinazotoa huduma za intaneti nchini humo, kufunga mitandao ya kijamii wakati uchaguzi mkuu, ukifanyika leo, nchini humo.

Museveni, akilihutubia taifa Jumanne usiku, alisema hawezi kuruhusu mtu kuichezea nchi hiyo.

Alisema matumizi ya mtandao wa Facebook yanastahili kutumiwa kwa usawa na kila mmoja.

"Mtandao huo wa kijamii, iwapo utatumika Uganda, lazima pawe na usawa, iwapo unaitenga NRM kwa kuifungia, basi kampuni hiyo haiwezi kufanya kazi Uganda.

Mtandao huo wa Facebook, serikali imeufungia, inasikitisha ila imebidi," alisema.

Jumanne, Tume ya Mawasiliano nchini Uganda, iliagiza kampuni za mawasiliano nchini humo, kufunga mawasiliano katika mitandao ya kijamii ya Twitter, WhatsApp, Instagram na Snapchat.

Hatua hiyo ya serikali ya Uganda, imelaaniwa vikali na Mwanadiplomasia wa Marekani kwa Bara la Afrika, Tibor Nagy, ambaye kwenye ukurasa wake wa twitter alisema kinachoendelea nchini humo ni ukiukwaji wa haki za watu.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Gutteres, alitoa wito kwa wanasiasa na wadau wote wa uchaguzi huo, kuhakikisha kuwa zoezi hilo linafanyika kwa utulivu.

Wakati huohuo, Polisi nchini humo, imedai Bobi Wine ana mpango wa kujiteka. Maofisa wa usalama walidai kuwa mgombea wa urais wa upinzani, Bobi Wine, anapanga kujiteka baada ya kupiga kura, ili kuchochea vurugu.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, Fred Enanga, alisema Bobi Wine hana mipango mizuri baada ya uchaguzi huo.

"Tuna habari za kuaminika kuwa Robert Kyagulanyi anataka kujificha baada ya kupiga kura, labda katika moja ya ubalozi wa nchi ya kigeni kisha baadaye aseme kuwa ametekwa, ili wafuasi wake waanze fujo, tunamwonya asijaribu kufanya hivyo," alisema Enanga.

Hata hivyo, madai hayo ya polisi yamekanushwa na Bobi Wine, ambaye alisema inaonekana kuwa maofisa wa usalama wanataka kumzuia nyumbani kwake.

"Sina sababu ya kujificha. Nitakuwa hapa nyumbani kwangu. Labda wanataka kunizuia nyumbani kwangu na ndio sababu wanasema hivyo," alisema Bobi Wine.

Aidha, jeshi la nchini humo, limetetea hatua yake ya kuwapeleka maofisa wake kwa wingi jijini Kampala na kukanusha kuwa kuna mpango wa kuwatisha wapigakura.


"Nimesikia watu wengi wakisema kwamba kwa nini wanajeshi ni wengi? Wametumwa kutokana na vitisho ambavyo tumepata.

Hatuna mpango wa kumtisha yeyote," alisema Brigedia Flavia Byekwaso, Msemaji wa Jeshi la UPDF.

Hali ya wasiwasi imezuka hasa jijini Kampala, kuelekea uchaguzi mkuu, ambao ushindani mkubwa ni kati ya kiongozi wa muda mrefu, Yoweri Museveni na mgombea kijana, Bobi Wine.

Wakati huo huo, Marekani imelaani uamuzi wa serikali kufunga mitandao ya kijamii, huku Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres akitoa wito wa kuheshimiwa haki za binadamu.

***RFI/BBC***



Mabaki ya ndege ya Sriwijaya Air SJ 182 yakiwa katika Bandari ya Tanjung Priok, Jakarta, Indonesia, baada ya ndege hiyo kuzama baharini mwishoni mwa wiki, ikiwa na abiria 62. Jana, Indonesia iliwasitisha wapigambizi kuendelea na uokoaji kufuatia hali ya hewa kuwa mbaya. **PICHA/REUTERS**

# Hali ya hatari yatangazwa kutokana na mafuriko

**Nis, SERBIA**

HALI ya hatari na ya dharura, imetangazwa kwa sababu ya mafuriko huko Nis, mojawapo ya miji mikubwa ya Serbia.

Miji mingine iliyotangaziwa hali ya hatari ni pamoja Leskovac, Doljevac, Bojnik, Vlasotnica, Vladicin Han na Gadzin Han.

Imetangazwa kuwa zaidi ya nyumba 10,000 na sehemu za kazi hazikuwa na umeme.

Taarifa iliyoandikwa na Idara ya Zimamoto ya Serbia, ilisema kwamba timu hizo zinaendelea na kazi zao katika maeneo yaliyoathiriwa na mafuriko, haswa katika maeneo ya kilimo.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Serbia, ilitangaza kuwa hali hiyo imedhibitiwa na kiwango cha juu cha maji katika mito kimeanza kupungua, wakati mvua ikipungua.

Katika taarifa iliyotolewa na Taasisi ya Hali ya Hewa ya Serbia, imeonya kuwa kiwango cha mtiririko wa Mto Lim ni cha hali ya juu.

***TRT***

## Mwanamke aliyekabiliwa adhabu ya kifo anyongwa Marekani

**Indiana, MAREKANI**

LISA Montgomery, ambaye alikuwa mfungwa pekee wa kike akikabiliwa na hukumu ya kifo nchini Marekani, amenyongwa.

Lusa, alidungwa sindano ya sumu katika Gereza la Terre Haute, Indiana, baada ya Mahakama ya Juu zaidi nchini humo, kuondoa agizo la kuzuia kunyongwa katika dakika za mwisho.

Kesi yake ilizua hisia kali baada ya mawakili wake kusema kwamba, alikuwa na tatizo la kiakili lililotokana na kunyanyaswa akiwa mtoto mdogo.

Mwanamke huyo aliyekuwa na umri wa miaka 52, alimnyonga mama mjamzito kabla ya kumkata tumbo na kumteka mtoto wake katika eneo la Missouri mwaka 2004.

Bobbie Jo Stinnett, aliyenyongwa alikuwa na umri wa miaka 23, alifariki baada ya kutokwa na damu nyingi.

Montgomery ni mfungwa wa kwanza wa kike nchini Marekani kunyongwa katika kipindi cha miaka 67 iliyopita.

Kwa mujibu wa walioshuhudia, mwanamke aliyekuwa amesimama karibu na Montgomery wakati wa kunyongwa kwake, huku akimwondoa barakoa aliyokuwa amevaa na kumuuliza ikiwa ana jambo la mwisho la kusema, Montgomery alijibu "la".

Hatua ya kunyongwa kwake iliahirishwa mara mbili, kwanza kutokana na janga la Covid-19 wakati huo na Jaji na Mahakama ya Juu zaidi, ilipotoa uamuzi wa kutekelezwa kwa hukumu hiyo mapema Jumatano.

Jumatatu jaji mjini Indiana, alisitisha ghafla kutekelezwa kwa hukumu hiyo hadi pale kesi ya kuchunguza hali yake ya kiakili ilipofanywa.

Mawakili wake walisema alizaliwa na ugonjwa ulioathiri ubongo wake na kuongeza kuwa alikuwa mgonjwa sana.

Akiwa mtoto alidhulumiwa kingono na baba yake, huku mama akimsafirisha kimagendo, jamaa za familia yake walisema.

Alipitia kipindi kirefu cha ghasia na mateso wakati wa utoto wake, mawakili wake walisema.

Montgomery alizuiliwa katika gereza la wanawake la Texas la wafungwa walio na mahitaji maalum, ambako amekuwa akipokea matunzo ya watu wenye matatizo ya afya ya akili.

Tangu tarehe ya kunyongwa kwake, ilipotolewa alifungiwa katika selo peke yake na amekuwa akifuatiliwa kwa karibu asijitoe uhai.

Desemba 2004, Montgomery, aliendesha gari kutoka Kansas hadi nyumbani kwa Bobbie Jo Stinnett, Missouri, akidaiwa kununua mtoto wa mbwa, kulingana na taarifa iliotolewa na idara ya sheria kwa vyombo vya habari.

"Baada ya kuingia nyumbani, Montgomery alimshambulia na kumnyonga Stinnett, ambaye alikuwa na ujauzito wa miezi nane, hadi mwathiriwa akapoteze fahamu," ilisema taarifa.

Montgomery alimkata tumbo mwanamke hiyo na kumtoa mtoto ambaye alimchukua na kudai kwamba ni wake.

Mwaka 2007, majaji walimpata Montgomery na kosa la utekaji nyara uliosababisha kifo na kwa kauli moja kutoa hukumu ya kifo dhidi yake.

Mawakili wake walisema alipata dosari kwenye ubongo kutokana na kupigwa akiwa mtoto na anaugua ugonjwa mbaya wa akili.

***BBC***



# LAMPARD KULETEWA GRANT CHELSEA

**LONDON, England**

MMILIKI wa Chelsea, Roman Abramovich, anafikiria kumrejea aliyewahi kuwa kocha wa timu hiyo, Avram Grant, kwa mujibu wa Daily Mail.

Abramovich anaamini uzoefu wa Grant utakuwa msaada mkubwa kwa kocha wa sasa wa Chelsea, Frank Lampard na benchi lake la ufundi katika kikosi hicho.

Chelsea wameshinda mchezo mmoja kati ya sita waliyocheza kwenye Ligi Kuu England wakiwa wanaendelea kudondosha pointi na sasa wameshuka mpaka nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

Grant alimnoa Lampard wakati alipokuwa kocha wa Chelsea na sasa anaandaliwa kwenda kumsaidia mchezaji wake huyo wa zamani.

Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti, Grant mwenyewe anaamini kwa uwezo wake, anafaa kuwa kocha wa timu na si kufanya kazi nyuma ya pazia.

Na hii inamaanisha kwamba, endapo atatua pale Stamford Bridge itakuwa ni kama anapita tu na si kufanya kazi kwa muda mrefu.

Grant aliiongoza Chelsea kumaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu wakati alipokuwa kocha wa timu hiyo.

# ANCELOTTI KUMRUDISHA KEAN EVERTON JUNI

**LIVERPOOL, England**

KOCHA Carlo Ancelotti amesema Moise Kean atarejea Everton Juni, lakini ikiwa atahitaji kuendelea kusalia na PSG basi mazungumzo zaidi yatahitajika kati ya pande zote.

Kean alijiunga na PSG kwa dili la mkopo Oktoba, lakini nyota huyo raia wa Italia anaweza kukamilisha uhamisho wa kudumu mwisho mwa msimu huu.

Kwa mujibu wa Sky Sport, PSG wapo katika makubaliano ya dili la milioni 35.

Akizungumza na Sky Sport, Ancelotti alisema nyota huyu anaendelea vema na anafurahia kuwapo PSG.

"Anafunga mabao mengi, anaonyesha ubora wake. Ni mchezaji wetu na atarejea Juni."



Aidha, alidai kuwa wakati wote klabu inapaswa pia kuzingatia yale ambayo yanafikiriwa na wachezaji, kwa kuwa nao ni binadamu.

Alisema ikiwa mchezaji anataka kurejea basi wao watafurahi kuendelea kuwa naye, kama atataka kuendelea kusalia PSG basi mazungumzo yatafanyika kati yao na PSG.

"Sihitaji mchezaji arejee wakati hafurahii kurejea. Kama mchezaji anafurahia kuja, anakaribishwa," alisema Ancelotti

Kean amefunga mabao 13 katika mechi 22 kwenye michuano yote msimu huu. Alijiunga na Everton kutoka Juventus kwa ada ya euro milioni 30 mwaka 2019.

# MKHITARYAN KUSAINI MKATABA MPYA ROMA

**ROME, Italia**

KLABU ya AS Roma imeripotiwa kuwa tayari imeshakamilisha mazungumzo na Henrikh Mkhitaryan na kufikia makubaliano ya kusaini mkataba utakaomweka hapo hadi Juni 2022.

Kwa mujibu wa taarifa zilizoripotiwa na vyanzo vya taarifa za mchezo ikiwamo Sky Sport Italia, Roma wanataka kumbakisha nyota huyo raia wa Armenia mwenye umri wa miaka 31, ambaye amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa klabu hiyo, Tiago Pinto.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, taarifa ya dili hilo inatarajiwa kutangazwa rasmi wiki zijazo na kuwa nyota huyu anasaini mkataba mpya utakaomshuhudia akiendelea kuwapo kikosini hapo hadi Juni 30, 2022.

Mkhitaryan amecheza mechi 17 za Serie A msimu huu, akifanikiwa kuchangia mabao nane na pasi za mwisho nane. Kiungo huyo aliwasili klabuni hapo kwa mkopo akitokea Arsenal Septemba 2020.

Bila shaka Roma wameridhishwa na kiwango chake dimbani na wanaona ni mtu ambaye anaweza kuwasaidia zaidi.

## HABARI MICHEZO



# DEPAY: NITABAKI LYON

**LYON, Ufaransa**

NYOTA wa Lyon, Memphis Depay, amesema anaweza kumaliza msimu akiwa na timu hiyo ya Ligue 1, wakati huu akihusishwa na Barcelona.

Depay ameendelea kuhusishwa na kutimkia Barcelona na mkataba wake utamalizika mwishoni mwa msimu huu wa 2020-21.

Raia huyo wa Uholanzi amebainisha kwamba, kuna uwezekano mkubwa akaondoka klabuni hapo, lakini hilo haliwezi kutokea sasa.

Wakati amekuwa akihusishwa na kuondoka, Depay amesema anaweza kumaliza msimu huu akiwa na Lyon.

"Nina furaha hapa. Tunatimu kubwa kiukweli nampenda rais, tutaona nini kitatokea,"aliiambia Canal+.

"Rais na mimi tunajua nini kilitokea katika misimu minne iliyopita, acha tuendelee kusonga na kufurahia uwapo wangu hapa, naweza kuwapo hapa hadi mwisho wa msimu huu.

Depay ametengeneza nafasi kubwa 10 na mshambuliaji wa Marseille, Florian Thauvin (12) na straika Angel Di Maria (11) waliotengeneza nafasi zaidi yake.

## LEWANDOWSKI ATAJA UBAYA WA KLOPP KWA UBORA WAKE

**MUNICH, Ujerumani**

ROBERT Lewandowski amezungumza kwa maneno mazuri juu ya uhusiano wake na Jurgen Klopp, akisema kocha huyo wa sasa wa Liverpool alikuwa "mwalimu mbaya" ambaye alimchochea kwenye njia ya kuwa bora.

Baada ya kupitia maisha magumu katika miaka yake ya utotoni, Lewandowski alianza kufunga mara kwa mara pale Znicz Pruszkow na Lech Poznan, ambayo ilimfanya ahamie Borussia Dortmund mwaka 2010.

Kuanza kwa maisha kwa Lewandowski kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, haikuwa rahisi, kwani alichezeshwa katika nafasi isiyojulikana na alipata maisha magumu kwenye mazoezi chini ya Klopp.

Akifafanua jinsi uhusiano wake na Klopp ulivyokuwa, Lewandowski aliliambia jarida la Bild: "Jurgen hakuwa kama baba tu kwangu. Kama kocha, alikuwa kama mwalimu "mbaya". Na ninamaanisha kwamba kwa maana bora ya neno.

"Acha nieleze. Fikiria nyuma yako wakati ulikuwa shuleni. Ni mwalimu gani unayemkumbuka zaidi? Si yule aliyekurahisishia maisha na hakutarajia chochote kutoka kwako.

"Hapana, hapana, hapana. Unakumbuka mwalimu mbaya, yule ambaye alikuwa mkali kwako. Yule aliyekupa shinikizo na alifanya kila kitu ili kupata kitu bora kutoka kwako. Huyo ndiye mwalimu aliyekufanya uwe bora, sivyo? Na Jurgen alikuwa hivyo.



## SOLSKJAER ACHOCHEA MOTO USHINDI UNITED

**LONDON, England**

OLE Gunner Solskjaer, amewasifu vijana wake wa Manchester United kuwa wana akili na juhudi kubwa ndani ya uwanja jambo ambalo linampa furaha kubwa kwa sasa.

Kocha huyo ameongeza kuwa ushindi ambao wameupata mbele ya wapinzani wao unawapa nguvu ya kuendelea kufanya vizuri kwenye mechi zao zijazo na anaamini watakuwa vizuri.

Man United ilishinda bao 1-0 dhidi ya Burnley kwenye mchezo wa Ligi Kuu England uliochezwa Uwanja wa Turf Moor na kuwafanya waongoze msimamo wa Ligi Kuu wakiwa na pointi 36 wakiwashusha mabingwa watetezi, Liverpool wenye pointi 33.

Bao pekee la ushindi lilifungwa na Paul Pogba dakika ya 71, ambaye aliibuka kuwa nyota wa mchezo huo.

"Vijana wamefanya kazi nzuri na kwa juhudi kubwa, hapo walipo wanastahili pongezi kwani sikutarajia kuona uwezo huo, imani yangu ni kwamba wataendelea kuwa bora muda wote ndani ya uwanja," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Nina imani kwamba mwamko na ari waliyonayo wachezaji wangu itaendelea katika kila mchezo uliopo mbele yetu.

"Dhamira yetu ni moja kwamba, tunataka ushindi kwenye kila mchezo na tunataka kuchukua taji msimu huu, na hilo naliona linakuja kwa sababu wachezaji wanaonyesha moyo wa kupambana na hawaonyeshi kuchoka katika hilo.

"Naamini mechi zetu zijazo, hasa mchezo dhidi ya Liverpool utakuwa mgumu, lakini lazima tupambane kwa nguvu zote."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA: TUPO TAYARI, WALETENI LIVERPOOL

●●● Utakuwa ni mchezo mzuri kwa kila mmoja, tunatakiwa kutulia, tutaona nini kitatokea...

**LONDON, England**

NYOTA wa Manchester United, Paul Pogba amesema 'Mashetani Wekundu' hao wapo tayari kuwavaa Liverpool, baada ya kupaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England.

United walikwea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kwa mara ya kwanza tangu msimu wa mwisho wa Alex Ferguson wa 2012-13 baada ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Burnley juzi, Jumanne.

Pogba alikuwa shujaa wa mchezo huo baada ya kufunga bao zikiwa zimesalia dakika 19 mpira kumalizika na kuwapeleka United kileleni mwa msimamo wakiwa wanaongoza kwa tofauti ya pointi tatu dhidi ya wapinzani wao, Liverpool, ambao watacheza nao Jumapili pale katika dimba la Anfield.

"Utakuwa ni mchezo mzuri kwa kila mmoja," alisema Pogba akiiambia BBC Sport, ambaye mabao yake matano kati ya saba yamepatikana kwenye mechi za ugenini.

"Ni mchezo mkubwa unaokuja na tupo tayari kwa hilo."

United ilitawala mchezo wakiwa nyumbani kwa Burnley na bao la Harry Maguire la kipindi cha kwanza lilikataliwa kwa madai ya faulo.

Lakini Pogba aliwapa ushindi Man United pale kwenye dimba la Turf Moor, akiunganisha vizuri krosi ya Marcus Rashford.

Rashford amehusika kwenye mabao 11 katika mechi zake 14 za Ligi Kuu zilizopita (mabao sita na pasi za mwisho tano) baada ya kumtengenezea Pogba juzi.

United sasa haijafungwa mechi 15 za ugenini kwenye Ligi Kuu tangu walipopoteza 2-0 kwa Liverpool, Januari mwaka jana.

"Tulijua kama tunataka kushinda, tunakwenda kileleni mwa msimamo wakati tutakapokwenda kucheza na Liverpool," alisema Pogba, ambaye kwenye mchezo huo aligusa mpira mara 106, akipiga pasi zilizokamilika 71.

"Tunatakiwa kutulia, sasa ni muda mkubwa kwetu. Tutaona nini kitatokea."

## KWA UFUPI

### MBAPPE KUUZA 6 MADRID
KLABU ya Real Madrid inapanga kuwauza wachezaji sita msimu huu ili kukusanya fedha za kumsajili mshambuliaji wa PSG, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22. Mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale, beki wa kushoto wa Brazil, Marcelo, Luka Jovic, Isco, Dani Ceballos na Brahim Diaz ndio wachezaji wanaolengwa. ***(AS)***

### GRANT KURUDI CHELSEA
MMILIKI wa Chelsea, Roman Abramovich, anafikiria kumrudisha kocha wa zamani, Avram Grant pale Stamford Bridge ili kumsaidia Frank Lampard. ***(Sky Sports)***

### FOSU-MENSAH KUTUA LEVERKUSEN
MLINZI wa Manchester United, Timothy Fosu-Mensah mwenye umri wa miaka 23, anatarajiwa kuhamia katika klabu ya Bayer Leverkusen kwa dau la pauni milioni 1.5 baada ya kukataa kuongezewa mkataba pale Old Trafford. ***(Manchester Evening News)***

### WOLVES KUMKOSA GIROUD
WOLVES haitamnyatia mshambuliaji anayelengwa na kocha, Nuno Espiroto, Olivier Giroud na yule wa Liverpool, Divock Origi mwenye umri wa miaka 25, baada ya klabu hiyo kumwambia kocha huyo kwamba haina fedha za kutumia Januari. ***(Mirror)***

### BAYERN YAMTAKA RICHARDS
KLABU ya Bayern Munich inatarajiwa kumsajili mlinzi wa Reading mwenye umri wa miaka 22, Omar Richards. ***(Guardian)***

### FERNANDINHO KUBAKI CITY
KIUNGO Fernandinho mwenye umri wa miaka 35, huenda akaongeza mkataba wake na Manchester City, kwa kuwa hana uhakika iwapo atakubali ofa kutoka Ulaya na Marekani mara mkataba wake utakapokamilika mwisho mwa msimu huu. ***(Telegraph)***

### NAPOLI KUMUUZA KOULIBALY
MLINZI wa Napoli, Kalidou Koulibaly anahusishwa sana na Liverpool, Manchester City na Manchester United - na atauzwa katika dirisha la uhamisho la mwezi huu iwapo timu inayomtaka itatoa ofa ya pauni milioni 100 kumnunua mchezaji huyo raia wa Senegal mwenye umri wa miaka 29. ***(Talksport)***

### CASEMIRO THAMANI KUBWA REAL
KIUNGO wa Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 28, ana thamani ya juu zaidi ya mchezaji yeyote yule wa Real Madrid, kwa mujibu wa ripoti ya wataalamu wa ukaguzi. ***(Mundo Deportivo)***

### MILAN YAMTAKA TOMORI
KLABU ya AC Milan inataka kumsajili mlinzi wa kati wa Chelsea, Fikayo Tomori kwa mkopo katika kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo. ***(The Guardian)***

### SLIMANI SASA KUTUA LYON
MSHAMBULIAJI wa Leicester City na Algeria, Islam Slimani mwenye umri wa miaka 32, anatarajiwa kujiunga na Lyon. ***(Sky Sports)***

### JOSEPH AGOMBEWA UINGEREZA
KLABU za Tottenham Hotspur, Sheffield United, Rangers na Celtic zote zinamnyatia mshambuliaji wa Wigan mwenye umri wa miaka 19, Kyle Joseph. ***(Mirror)***

## HABARI MICHEZO

# LYANGA AZUNGUMZIA BAO LAKE TAIFA STARS

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa timu ya Taifa (Taifa Stars), Ayoub Lyanga, ameonyesha furaha kubwa kufunga bao lililoifanya timu hiyo kuepuka kipigo dhidi ya wageni wao Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) katika mechi ya kirafiki iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1.

Lyanga anayeichezea Azam FC, alisema bao hilo ambalo limewafanya Watanzania wasitoke kichwa chini kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, limemfurahisha yeye binafsi na litamfanya kuongeza juhudi zaidi kwenye fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN.

"Nimejisikia furaha sana kwa sababu nimeifungia Tanzania. Hii imenisaidia mimi na wenzangu kujiamini na kujiweka vizuri kwenye michuano ya CHAN. Ni michuano mikubwa, lakini mimi nimejiandaa kuendelea kuifungia timu yangu mabao na pia wenzangu wamejiandaa ili tufanye vizuri," alisema Lyanga.

Winga huyo alifunga bao hilo dakika ya 51 kwa kichwa baada ya kuunganisha mpira wa krosi uliopigwa kutoka kwa Ditram Nchimbi, akisawazisha goli la dakika ya 19 lililofungwa na Fiston Mayele.

Ilikuwa ni mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyo kwenye Kalenda ya FIFA, timu zote mbili zikijiandaa na fainali za CHAN inayotarajiwa kuanza Januari 16 hadi Februari 7, mwaka huu nchini Cameroon.

Wakati Stars iko Kundi D na timu za Guinea, Namibia na Zambia, DRC, iko Kundi B sambamba na Congo Brazzaville, Libya na Niger.

DRC itaanza kucheza mechi yake ya kwanza Jumapili dhidi ya 'ndugu zao' wa Congo Brazzaville, wakati Stars itaingia uwanjani kwa mara ya kwanza Jumanne, ikicheza dhidi ya Zambia 'Chipolopolo'.

**WAMETUSUA...**




Msemaji wa Kampuni ya M-Bet Tanzania, David Malley (katikati), akiwa na washindi watano wa droo ya Perfect 12 walioshinda kwa kubashiri kwa usahihi matokeo ya michezo 12 kati ya 17 ya ligi mbalimbali duniani. **MPIGAPICHA WETU**

# M-BET yawajaza mamilioni washindi wake

**Na Mwandishi Wetu**

MASHABIKI watano wa soka nchini wameshinda kiasi cha Sh. milioni 86.8 baada ya kubashiri kwa usahihi jumla ya mechi 12 kati ya 17 za ligi mbalimbali duniani kupitia droo ya Perfect 12 inayochezeshwa na Kampuni ya M-Bet, imeelezwa.

Washindi hao wamepatikana katika droo ya M-Bet iliyofanyika Januari 6, mwaka huu jijini Dar es Salaam, Msemaji wa M-Bet Tanzania, David Malley amesema. Malley aliwataja washindi hao ni pamoja na Charles Hamis kutoka Lindi, Isihaka Mombo, Titus Mguli wote kutoka mkoani Njombe, Eric Mosha wa Tanga na Baltazary Saunary wa jijini Arusha.

Malley alisema kupatikana kwa washindi hao kunafanya idadi ya droo kufikia 101 tangu kuanzishwa kwa Pefect 12 ambayo ni 'Nyumba ya Mabingwa'.

Alisema M-Bet inajivunia kuendelea kubadili maisha ya Watanzania kupitia michezo yake mbalimbali na kuwataka mashabiki wenye vigezo vya kufanya hivyo kuendelea kujaribu bahati yao.

Mmoja wa washindi hao, Charles Hamisi, kutoka Lindi alisema amefurahi sana kushinda kiasi hicho cha fedha kwa kutumia mtaji wa Sh. 1,000.

Hamisi ambaye shabiki wa Simba na Manchester United alisema awali alidhani michezo ya kubahatisha ni 'maigizo' lakini baada ya kuona mashabiki kibao wakishinda kupitia M-Bet, naye aliamua kubashiri.

## Ligi Kuu Z'bar kurejea na dirisha dogo Jan. 22

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kumalizika kwa mashindano ya Kombe la Mapinduzi jana usiku, Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), limetangaza Ligi Kuu visiwani hapa itarejea tena kuanzia Januari 22, mwaka huu kwa JKU kuwakaribisha Black Sailor kwenye Uwanja wa Mau A.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Kuu Zanzibar, Sheha Mohamed Ali, alisema ratiba inaonyesha ligi hiyo itaendelea kwa mechi za mzunguko wa kwanza zilizobaki na baada ya hapo watafungua dirisha dogo la usajili.

Ali alisema wakati ligi hiyo inayoshirikisha klabu 12 inasimama kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi, kila timu ilikuwa imecheza mechi nane.

Kiongozi huyo alitaja mechi nyingine zitakazochezwa siku hiyo ni pamoja Kipanga dhidi ya Chuoni kwenye Uwanja wa Amaan wakati wenyeji Hard Rock watawakaribisha Malindi kwenye Uwanja wa Gombani ulioko Pemba.

Alisema kwa upande wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, yenyewe itaanza kuchezwa kuanzia Jumamosi Januari 16, mwaka huu na ratiba yake itatolewa wakati wowote kuanzia leo.

"Kamati iko ipo katika hatua za mwisho za kuifanya marekebisho ratiba ya Ligi Daraja la Kwanza, tutaitoa mapema ili klabu zifahamu mechi zao," alisema kiongozi huyo.

## Betika yaendelea kutajirisha wadau

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya michezo ya kubahatisha ya Betika imetoa washindi 24 ndani ya wiki moja katika Jackpot yake ya 'Kitonga Deile' inayofanyika kila siku.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Kitengo cha Fedha wa kampuni hiyo, Deodata Kalumia, alisema kila siku wanatoa mshindi anayejinyakulia Sh. milioni moja.


"Mambo yanazidi kuwa matamu kila siku ni mpya, na sasa ushuhuda huu unadhihirika hadharani baada ya washindi 24 ndani ya wiki moja kujizolea 'mapesa' yao ndani ya Jackpot, hii haijawahi kutokea kwingine," alisema na kuongeza kuwa; "Betika inataka wewe ushinde na uzidi kuongeza idadi ya washindi wengine katika Kitonga Deile Jackpot ambayo inakuwezesha kushinda Sh. 1,000,000 kila siku, na kuifanya Januari yako kuwa nyepesi kwa kushiriki na kuchagua mechi nane tu, kisha weka ubashiri ukitumia dau la Sh. 250 tu na maisha yako yatabadilika kwa kujishindia fedha hizo," alisema Kalumia.

Aliongeza kwa kuwataka mashabiki wote wa soka kuichagua Betika ili kurahisisha maisha yao kwa kupata zawadi zinazotolewa kila siku endapo watabashiri kwa usahihi.

# Michezo

Alhamisi Januari 14, 2021

Nipashe

POGBA: TUPO TAYARI, WALETENI LIVERPOOL

HABARI UK 22

MWALI WENU...



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kushoto), akimkabidhi Kombe la Mapinduzi, nahodha wa Yanga, Haruna Niyonzima, baada ya kuifunga Simba kwa penalti 4-3 kwenye mechi ya fainali ya michuano hiyo iliyopigwa Uwanja wa Amaan jana. Timu hizo zilitoka suluhu ndani ya dakika 90. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# YANGA BINGWA

●●●Yabeba Mapinduzi Cup Mnyama akifia tutani Uwanja wa Amani, Kahata mchezaji bora, Onyango naye...

**Na Adam Fungmwangwo**

BAADA ya miaka 17, timu ya Yanga imefanikiwa kutwaa Kombe la Mapinduzi kwa kuwafunga mahasimu wao wa jadi Simba kwa mikwaju ya penalti 4-3, baada ya kutoka suluhu ya bila kufungana kwa dakika 90 kwenye Uwanja wa Amaan Zanzibar.

Mara ya mwisho Yanga kutwaa kombe hilo ilikuwa ni mwaka 2007 kwenye uwanja huo ilipoifunga Mtibwa Sugar mabao 2-1.

Penalti ya Meddie Kagere iliyogonga 'mtambaa panya' na Joash Onyango kupanguliwa na kipa Farouk Shikalo, iliwafanya mashabiki wa Simba kutoka uwanjani vichwa chini na kuwaacha wenzao wa Yanga wakikabidhiwa kombe hilo na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Penalti za Yanga zilikwamishwa nyavuni na Tuisila Kisinda, Abdallah Shaibu 'Ninja', Zawadi Mauya na Saido Ntibazonkiza, huku ya Mukoko Tonombe ikipanguliwa na kipa Beno Kakolanya. Kwa upande wa penalti za Simba ziliwekwa nyavuni na Francis Kahata, Chris Mugalu na Gadiel Michael.

Hii ni mara ya pili kwa timu hizo kukutana kwenye fainali ya kombe hilo, kwani 2011 zilikutana na Simba kushinda mabao 2-0, yaliyofungwa na Mussa Hassan Mgosi na Shija Mkina.

Kadhalika, hii ni mara ya tano kwa Simba kufungwa kwenye hatua ya fainali ya michuano hiyo iliyofanikiwa kulichukua mara tatu, mwaka 2008 ilipoifunga Mtibwa Sugar fainali kisha 2011 ikaifunga Yanga na 2015 ikaifunga tena Mtibwa kwa penalti 4-3.

Katika mechi ya jana, dakika ya sita tu ya mchezo, nusura Yanga ijifunge baada ya shuti la Hassan Dilunga kumbabatiza Tuisila Kisinda na kugonga nguzo, lakini kwa bahati nzuri ulitoka nje na kuwa kona tasa.

Dakika tatu baadaye, Yanga ilifanya shambulizi kali langoni mwa Simba, baada ya Ntibazonkiza na Haruna Niyonzima kugongana ndani ya eneo la hatari, lakini kabla Niyonzima kuukwamisha wavuni, Gadiel Michael aliuokoa.

Yanga ambayo ilitawala karibuni dakika zote 30 za kipindi cha kwanza, almanusura ipate bao dakika ya 25, baada ya faulo ya Ntibazonkiza kuunganishwa kwa kichwa na Michael Sarpong, mpira huo ulimbabatiza kipa Beno Kakolanya na kuzua kizaazaa golini mwa Simba, kabla ya kipa huyo kuurukia na kuudaka.

Simba ilionekana kuzinduka dakika 15 za mwisho za kipindi cha kwanza na dakika ya 38, Joash Onyango ambaye jana alitangazwa kuwa mchezaji bora wa mechi hiyo ya fainali, aliunganisha kona iliyopigwa na Francis Kahata mpira ukatoka sentimeta chache langoni mwa Yanga.

Yanga ilikosa tena bao dakika moja kabla ya mapumziko, baada ya Tuisila kumlamba chenga David Kameta kwenye wingi ya kushoto na kutoa krosi pasi kwa Sarpong ambaye badala ya kupasia nyavu, alipiga nje.

Kipindi cha pili timu zote zilicheza mchezo wa kutumia nguvu zaidi na kushambuliaji na kushtukiza, hadi dakika 90 zilipokamilika na kulazimika kupigiana mikwaju ya penalti.

Aidha, Kahata alitangazwa kuwa mchezaji bora wa mashindano hayo huku Simba ikitangazwa kuwa timu bora.

## IBENGE AJITOA SIMBA, AITANGAZIA VITA CAF

**Na Adam Fungamwango**

HUKU akitajwa kuwa miongoni mwa makocha watatu wanaopewa nafasi kubwa ya kurithi mikoba ya Sven Vandenbroeck katika kikosi cha Simba, Kocha Mkuu wa timu ya AS Vita ya DR Congo, Jean-Florent Ibenge, amejiweka kando baada ya kueleza kuwa hajazungumza lolote na mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara na anachowaza ni mechi dhidi yao ya hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika.

AS Vita itaikaribisha Simba katika mechi ya kwanza ya hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika itakayopigwa DR Congo Februari 12, kabla ya timu hizo kurudiana Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kati ya Aprili 2-3, mwaka huu.

Ibenge ambaye ni Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya DR Congo, baada ya mechi ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya Taifa Stars iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1 juzi katika Uwanja wa Mkapa, Nipashe lilitaka kujua kuhusu tetesi hizo za kuja kuinoa Simba, ambapo aliweka wazi kuwa hakuna chochote kinachoendelea kati yake na Simba kwa sasa.

"Mimi ni Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya DR Congo na nakwenda nayo kwenye CHAN (Michuano ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani), kwa hiyo haiwezekani kwenda kuifundisha timu ya taifa, halafu hapo hapo nikaja kuifundisha Simba. Lakini mimi ni kocha wa AS Vita, kwa hiyo hayo yote yanayoongelewa ni uvumi tu," alisema kocha huyo ambaye timu yake ya AS Vita kwenye Ligi ya Mabingwa iko Kundi A pamoja na Simba, Al Ahly ya Misri na Al-Merrikh ya Sudan.

Lakini aliweka wazi kuwa yeye ni kocha, hivyo inawezekana kwa siku za baadaye kuja kufundisha hapa nchini na siyo kwenye klabu ya Simba tu, bali hata Yanga na Azam ambazo nazo ni klabu kubwa nchini Tanzania.

Kuhusu mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika hatua za makundi, alisema zitakuwa ngumu kwa timu yake ya AS Vita hasa kwa Al Ahly na Simba, lakini lengo lake ni kuwa moja kati ya timu mbili zitakazokwenda robo fainali.

Kocha huyo alisema licha ya kuwafunga Simba mabao 5-0 walipokutana DR Congo, lakini walishindwa kufuzu hatua ya robo fainali baada ya kupoteza hapa nchini, hivyo mwaka huu wamepania kupata matokeo nyumbani na ugenini.

Mbali na Ibenge, makocha wengine wanaopewa nafasi kubwa kuinoa Simba baada ya Sven kuachia ngazi na kujiunga na FAR Rabat ya Morocco ni Kocha wa zamani wa Al Ahly ya Misri raia wa Uswisi, Rene Weiler na Kocha Msaidizi wa Raja Casablanca ya Morocco, Hicham Aboucherouane.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042